**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |
| **Ndugu Yahya Khamis Hamad** | **Katibu wa Baraza la Wawakilishi** |

**Kikao cha Kumi na Sita - Tarehe 5 Juni, 2015**

*(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI**

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2015/2016. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka Hati Mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2015/2016. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 14**

**Tatizo la Msongamano wa Magari**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma)** - Aliuliza:-

Mhe. Spika, ahsante kwa niaba ya Mhe. Saleh Nassor Juma, ambaye amemaliza muda wake wa kukaribia Uwawakilishi kwenye Jimbo la Wawi, naomba swali lake Nam. 14 lipate jawabu.

Kwa kuwa harakati za maendeleo Zanzibar, zimesababisha kuwepo kwa ongezeko kubwa la magari kiasi cha kusababisha msongamano mkubwa hususan katika siku za siku kuu za Kidini pamoja na Sherehe nyengine za Serikali, hasa katika maeneo ya Darajani, Forodhani, Michenzani, Kisiwandui na kadhalika.

Je, ni hatua gani za dharura zilichukuliwa au zilizochukuliwa na SMZ  katika kupunguza msongamano wa magari katika siku hizo muhimu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma, swali lake Nam. 14 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika siku za Sikukuu kunakuwa na msongamano mkubwa wa magari katika maeneo mbali mbali ya mji wa Zanzibar na hali hiyo inatokana na wingi wa magari na uhaba wa maegesho katika maeneo ya mji wa Zanzibar.

Hata hivyo, Serikali kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi inachukua hatua madhubuti na za dharura kwa kusimamia kadhia hiyo kwa muda wote wa siku kuu ili kupunguza msongamano unaojitokeza katika siku hizo za siku kuu.

Mhe. Spika, itaendeleza mpango mkubwa wa upangaji wa mji wa Zanzibar ambao kwa kiasi kikubwa utaondoa tatizo hili liliopo hivi sasa.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza mawili madogo ya nyongeza.

1. Mhe. Naibu Waziri, utakubaliana na mimi kwa kiasi fulani Serikali inachangia huu msongamano na kama utakataa nipo tayari kukuthibitishia kuwa msongamano huu wa magari Serikali inachangia kwa kiasi fulani.

2. Serikali ina mpango wa kuendeleza mpango miji, huu wimbo umekuwa muda mrefu na huu mziki umekuwa ukipigwa kwa muda mrefu. Ni lini hadithi hii itamalizika ili kujua ukweli wa kadhia hii.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano**: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, maswali yake mawili ya nyongeza kwa pamoja kama ifuatavyo.

1) Mhe. Spika, kwanza sikubaliani na Mhe. Mwakilishi, kusema kwamba Serikali inachangia au inasababisha kuwepo kwa foleni.Ninaamini kwamba madhumuni ya Serikali ni kuona wananchi wake wanaishi kwa raha na mustarehe na kama kuna matatizo ni wajibu wetu Serikali kutafuta namna ya kuondoa changamoto zinazojitokeza.

2) Suala hili anauliza Serikali itakamilisha mpango wa mji. Mhe. Spika, suala la mipango miji na utekelezaji wake ni sawa endelevu. Tutapanga leo tutajenga na yeye mwenyewe ni shahidi yapo maeneo ambayo

yamepangwa siku za karibuni Mji wa maendeleo Mji wa Mombasa unatofautiana na Mji wa Kwahani, Kwaalinatu. Kwa hivyo, Serikali katika suala la upangaji wa mji ni suala endelevu. Tunachokizungumza hapa ni kupanga kwa ajili ya kuongeza maeneo mengi na makubwa kwa ajili ya kukidhi maegesho kutokana na mweendelezo na uongezekaji wa idadi ya magari na matumizi yake.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, ninataka nimuulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inakuwa na mipango madhubuti katika kuhakikisha msongamano hakuna na wakati ilipoanzisha Kituo cha Daladala cha Michenzani kilianzia na utaratibu wa kuweka vituo vidogo vidogo kwa Binti Hamrani na Uwanja wa Demokrasia.

Je, suala lile limefikia wapi au tatizo ni nini lilopelekea watu kutokuvitumia vituo vile.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Salum Haji, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, suala la uwekaji wa vituo vya Daladala ni suala mtambuka, suala ambalo Serikali lazima tushirikiane na wadau binafsi hasa wamiliki wa magari, kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Tawala na Mikoa na Idara Maalum SMZ, tushirikiane na wenzetu wa Manispaa kwa maana kwa pamoja na Madiwani ili tuweze kupata meneo husika.

Katika maeneo haya ambayo yametengwa hivi vituo kuna haja ya kutengeneza miunombinu maalum ya kuweza kukidhi watumiaji wa barabara kwa maana ya kwamba hivyo vituo. Kwa mfano maeneo ambayo yanatengenezwa vituo kunatakiwa angalau kuwe na eneo la kuweza kufanya kivuli lakini pia kuwe na maeneo unaweza ukapata sehemu ya kwenda kujisaidia kwa karibu.

Lakini haya yote yanatokana na mpango mkubwa wa Serikali wa upangaji wa mji, lakini pia katika mpango wetu wa mradi wa barabara zinazoingia mjini tutatengeneza sehemu maalum kwa ajili ya kuweza kuchukua vituo na vituo na watu wanaotumia barabara kwa matumizi yote. Kwa maana ya kwamba wale *pedestrians*, walemavu, maeneo ya maegesho na watu wengine wataweza kutumia barabara katika mradi utakapokamilika.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, lakini katika maongezi yake alisemea suala la wadau kuweza kukaa pamoja na kuweza kuangalia uwezekano wa kuweza kutafuta huo mustakabali wa tatizo ambalo lipo mbele yetu.

Sasa je, Serikali ina mpango gani katika kuhakikisha kwamba hilo linafanyika ili kuweza kutatua tatizo ambalo limetuzidia katika nchi yetu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Serikali kwa maana ya kwamba Wizara yangu katika sekta yanayohusiana na masuala ya usafiri tunakutana na wadau takriban mwaka mara mbili. Tunachokizungumza hapa ni uendelezaji wa maeneo kwa ajili ya maegesho. Hili lazima tukutane na wadau na tumesema hilo ni suala mtambuka.

Lazima tukutane sisi Serikalini, siyo tu Wizara yetu pamoja na wenzetu wanaohusiana na masuala ya Tawala za Mikoa. Lakini pia tuandae hiyo miundombinu kwa ajili ya kuweza kuchukua hayo matumizi yanayokusudiwa na tukasema kwamba tunagemea kwamba tutakapoweza hilo na tutakapokamilisha mradi mkubwa wa barabara zinazoingia mjini tutatenga maalum kuweza kuweza kuwa-*accommodate* hiyo hali ambayo ipo hivi sasa.

Kwa hivyo, suala la kukutana na wadau kwetu sisi ni kila kipindi angalau mara mbili kwa mwaka kwa kuweza kufanya hivyo. Lakini kwa mambo mengine haya ya matumizi ya barabara tunakuwa tunakutana nao na tunafanya semina na ninaamini hata kesho tuna mpango kama huo wa kukutana na wadau kwa ajili ya kuboresha matumizi mazuri ya magari, matumizi mazuri ya barabara na watumiaji wake. Kwa kuondoa hiyo misongamano ambayo inajitokeza barabarani.

**Mhe. Spika:** Huyo bwana ana tabia ya kukimbia huyo. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum SMZ, majibu ya nyongeza.(*Kicheko*)

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum SMZ:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kutoa majibu ya nyongeza na vile vile kwanza kabisa ninataka nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa majibu mazuri mwanana yenye uhakika ambayo amejibu kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu masuala yao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninataka niseme kwamba Serikali kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano katika sekta hii ya usafiri wa barabarani ili iweze kufanikiwa vizuri ni lazima wadau au wahusika wote waweze kukutana mara mbili kwa mwaka.

Mhe. Spika, Serikali tayari imeshafanya jambo hilo la kukutana na wahusika wote; sekta ya usafiri wa barabarani, Baraza la Manispaa, wenzetu wa Jeshi la Polisi, Wamiliki wa Daladala na Chama cha Wenye Daladala. Kazi hii ilikuwa iwe imekamilika mapema ndani ya mwaka huu wa bajeti, lakini itakumbukwa kwamba kupitia Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi ilitaka lazima Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nao wahusishwe ili na wao waweze kutoa maoni yao.

Ndiyo maana Serikali kwa kushirikiana na Baraza la Wawakilishi imeandaa semina kesho wakiwa ni sehemu ya wadau juu ya jambo hili. Kwa hivyo, ionekane kwamba Serikali inafanya hiyo kazi na ilikuwa iwe imemalizika mapema, lakini kwa sababu ya kuwashirikisha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hii kazi ikawa haijakamilika.

Kwa hivyo, ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi washiriki kesho ili watoe maoni yao na hatimaye Serikali iweze kuchukua hatua ya kuweza kuwaondoshea wananchi kadhia hii ambayo ipo.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Tunakushukuru Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri, sasa muache akakae kitako. Tunaendelea.

**Nam. 66**

**Ununuzi wa Majenereta**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Alijibu:-

Serikali ya Mapnduzi ya Zanzibar iliamua kwa nia njema kuwa na Kituo chake cha Umeme wa dharura baada ya Zanzibar kukosa umeme kwa miezi mitatu (3) kufuatia kuripuka kwa waya unaopeleka umeme kutoka Tanzania Bara katika Kituo cha Fumba. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sasa jenereta hizo zilizofungwa zimebakia kuwa mapamba.

a) Kwa nini Serikali ikanunua kitu ambacho hakina uwezo kukitumia na hatua hiyo siyo matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi na wahisani.

b) Kwa kuwa jenereta hizo hukaa bila ya kufanya kazi na Serikali inaendelea kupata hasara, kwa nni jenereta hizo zisiuzwe na fedha itakayopatikana zikatumika katika maendeleo ya Shirika badala ya kuendelea kuliwa na kutu na Serikali kuendelea kuzihudumikia bila ya kuzalisha.

c) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa watu walionunua jenereta bila ya kufanya uchambuzi yakinifu na kusababisha hasara kubwa ikiwemo kurudisha nyuma Zanzibar kimaendeleo badala ya kusonga mbele.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** - Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante sana kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 66 kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, ununuzi wa majenereta hayo ulisimamiwa kwa sehemu kubwa na Mshauri Mwelekezi Kampuni ya Norplan iliyoteuliwa na Serikali na Norway iliyoachiwa jukumu la kushughukia ununuzi huo na washirika wengine wa maendeleo waliochangia fedha za majenereta hayo ni Serikali ya Uingereza, Serikali ya Sweden na Mshauri Mwelekezi huyo ndiye aliyeongoza mchakato wa ununuzi wa majenereta hayo.

Mhe. Spika, kutokana na kukosekana kwa aina nyengine ya majenereta na umuhimu wa kupatikana kwa majenereta kwa haraka ndiyo ununuzi wa majenereta hayo ulifanyika.

Mhe. Spika, madhumuni makuu ya majenereta hayo ni kutumika wakati wa dharura ya kukosekana kwa umeme kupitia waya wa baharini katika kipindi ambacho dharura hiyo inapotokezea majenereta hayo basi hutumika na pale ambapo dharura hiyo haijatokezea, basi majenereta hayo hayatumika.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu ya awali niliyotanguliza kuelezea Serikali haioni sababu ya kumchukua hatua mtu yeyote katika ununuzi wa majenereta kwa vile ununuzi wake ulifanyika kwa lengo jema kabisa.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kutokuwa na afya wala kiwango na majibu ya kusikitisha kabisa. Naomba kumuuliza maswali mawili madogo sana ya nyongeza.

1) Mhe. Naibu Waziri, ulipokuwa ukijibu swali la msingi unasema majenereta hayo wakati unapotokea dharura huwa yanatumika ambacho kitu hicho si kweli na dharura mara nyingi zinatokea na majenereta hayo hajawahi kutumika,

inachukua masaa mpaka wakati kutwa kama Jumamosi umeme haujawashwa na hatujashuhudia kutumika umeme huo.

Je, unawaambia nini wananchi kauli uliyoitoa hapa ni ya kweli au ni uwongo. Na kushindwa kwa majukumu yako, ni lini utajiuzulu baada ya kutokusimamia majukumu yako vizuri.

2) Majenereta hayo umesema yamenunuliwa kwa dharura baada ya kukosekana mwengine. Je, unaweza kuliambia nini Baraza hili pamoja na wananchi *running cost* yake kwa siku ni shilingi ngapi majenereta hayo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, ahsante sana kwa niaba yake naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza kama hivi ifuatavyo.

1. Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba majenereta haya hutumika pale wakati inapotokea dharura, lakini vile vile Mhe. Mwakilishi atofautishe katika shughuli ndogo ndogo za kukatwa umeme kwa ajili ya matengenezo madogo na dharura. Hivyo ni viwili tofauti. Kwa hivyo, majenereta hutumika kwa dharura.

2. Mhe. Spika, vile vile katika suala la bei ya umeme kupitia majenereta haya. Mhe. Spika, nimuhakikishie kwamba kama tutatumia majenereta haya kwa sasa hivi basi *cost* ya *unit* ya umeme itakuwa kubwa zaidi, kwa sababu *cost* yake kwa kila *unit* moja pindipo tutakapotumia majenereta haya basi inachukua shilingi mia sita kwa *unit* moja. Kwa hivyo, kwa kuyatumia tu bila ya dharura majenereta hatuwezi kuyatumia.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali japo dogo tu la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa majenereta yale tumenunua na badala yake hatukuweza kufikia malengo ambayo ilikuwa tumeyakusudia.

Vile vile, ukizingatia dunia sasa hivi imeendelea na kuna utaratibu wa kuweza kufanya mabadiliko, kutoka matumizi ambayo tunatumia sasa hivi kwa majenereta yale kutumia mafuta ya *diesel*, tukaweza kutumia gesi au hata *battery* kama ambavyo wataalamu wengine wanakuwa watuelezea.

Sasa je, serikali ina mpango gani wa kitaalamu kuweza kutumika, ili majenereta yale yakaweza kuendelea kutumika kwa faida ya wananchi katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati:** Ahsante Mhe. Spika, ni kweli. Kwanza nataka aelewe Mhe. Mwakilishi kama nilivyoeleza pale awali kwamba majenereta yale pindipo tukiyatumia yana gharama kubwa mno ukilinganishana na mafuta yake.

Kwa hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia Baraza la Mapinduzi, imetoa agizo rasmi kwamba majenereta yale tuyauze kwa maslahi ya umma, na tutafute njia nyengine ya kuweza kuweka vyombo vya dharura ambavyo vinaweza kutusaidia. Kwa hivyo, serikali imeshaamua rasmi majenereta hayo yauzwe. Kwa sasa wizara yangu kwa kupitia Shirika la Umeme inasubiri wateja tu, watakapotokea tutawauzia majenereta hayo na tutafute mpango mwengine wa kufanya kwa ajili ya kuweka vitu vya dharura vya kuweza kutumia, pindipo litakapotokezea tatizo. *(Makofi)*

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali moja dogo la nyongeza Mhe. Naibu Waziri. Kwa kuwa amesema kwamba serikali kwa kupitia Baraza la Mapinduzi, limeshaidhinisha kwamba majenereta yale yauzwe. Na kwa kuwa Naibu Waziri, amesema kwamba hivi sasa wanachosubiri ni wateja tu.

Je, serikali imeshatoa tamko rasmi la matangazo katika vyombo husika vya kutangaza kuuzwa kwa majenereta yale. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Ahsante Mhe. Spika. Mhe. Spika, serikali kwa kupitia wizara yangu na Shirika la Umeme tayari wameshatoa tangazo. Na wamewahi kutokezea wateja na kuja kuangalia, tukakubaliana vizuri, lakini baadae wateja wale hawakurudi tena na wamekuja baada ya kuipata taarifa rasmi kwamba majenereta yale yanauzwa. *(Makofi)*

**Nam. 22**

**Kipimo Kinachotumika Kufanya Tathmini ya Mitihani**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma)** - Aliuliza:-

Kwa kuwa shule za binafsi (*Private*) hapa Zanzibar zimejitahidi sana kutoa elimu kwa watoto wetu kwa umakini mkubwa. Na kwa kuwa katika shule hizi wanafunzi wake hufanya mitihani yote ya Zanzibar na ile ya Jamhuri ya Muungano, kwa maana *STD 7* na *Form II* katika Baraza la Mitihani la Zanzibar na *Form IV* na *Form VI* kutoka Baraza la Mitihani la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (*NEC*). Na kwa kuwa baada ya kumalizika mitihani taasisi hizi mbili hutoa tathmini ya ufaulu wa wanafunzi pamoja na shule zilizofanya vyema mitihani yake.

Je, ni kipimo gani kilichotumika katika Baraza la Mitihani la Zanzibar hata likatoa matokeo kwamba shule ya *Connecting* iliyoko Mgogoni katika Jimbo la Wawi ni ya mwisho katika kufaulu wanafunzi wa Kidato cha Pili kwa mwaka wa 2014/2015 huku wanafunzi wote waliotahiniwa ni 63 na waliofaulu ni hao hao 63.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba sasa kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 22. Kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa skuli binafsi zinachangia sana katika utowaji wa elimu bora kwa wanafunzi wetu. Pia, ni kweli kuwa kuanzia mwaka 2014 wanafunzi wote wa Kidato cha Pili wa skuli za serikali na za binafsi walifanya mitihani ya pamoja ya Kidato cha Pili, kwa lengo la kutathmini kiwango cha elimu cha wanafunzi wetu wote wa Zanzibar. Mhe. Spika, hatua kama hiyo imekuwa ikifanyika kwa mitihani ya taifa ya Kidato cha Nne na cha Sita.

Vile vile, ni kweli kuwa katika mitihani ya pamoja ya Kidato cha Pili kwa mwaka 2014, wanafunzi wote 63 wa skuli *Connecting Continent* ilioko Wawi Wilaya ya Chake Chake Pemba walifaulu mitihani yao. Hata hivyo, napenda kukiri kufanyika kwa makosa katika utoaji wa matokeo ya mitihani ya Kidato cha Pili kwa mwaka 2014, ambapo skuli hiyo ilitangaza kuwa ni miongoni mwa skuli ambazo zilifanya vibaya, jambo ambalo halikuwa sahihi.

Mhe. Spika, baada ya kutangazwa matokeo, wizara ilipokea barua ya malalamiko ya skuli ya *Connecting Continent* ya tarehe 28 Januari, 2015 na ilipokelewa na wizara tarehe 04 Februari, 2015. Wizara iliagiza Baraza la Mitihani la Zanzibar kulifanyiakazi suala hilo na kugundua makosa ambayo yalifanyika katika kupata wastani wa Kiskuli, na hivyo Baraza liliangalia upya matokeo kwa wastani wa kiskuli katika uchunguzi huo, Baraza liligundua kama ifuatavyo:-

I) Wanafunzo wote 63 wa Skuli hiyo walifaulu mitihani yao.
II) Alama za wastani katika masomo yake yote zilikuwa ni sahihi.
III) Wastani wa masomo kwa watahiniwa wa skuli hiyo ilikuwa ni 44.0 na nafasi ya skuli hiyo ilikuwa ni ya 21 katika skuli 155, kwa skuli zilizokuwa na watahiniwa zaidi ya 45.

Mhe. Spika, wizara inaomba radhi kwa wanafunzi, walimu na wazazi wote wa wanafunzi wa skuli hiyo, kwa kosa hilo ambalo lilifanyika bila ya kukusudia.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika. Kwanza nichukuwe fursa hii kumshukuru Naibu Waziri kwa umakini wake na kukiri. Niwaombe Manaibu

Waziri wengine wawe mfano kwake yeye, kwa kueleza ukweli na kukiri kwa suala hili na kuomba radhi.

Mhe. Spika, mimi nichukuwe fursa hii kwanza kuwapongeza wanafunzi wa Skuli ya *Connecting Continent* kwa wote 63 kwa kufaulu, niwapongeze kwa dhati pamoja na walimu wao na jitihada zao.

Swali Mhe. Naibu Waziri, kwa kipindi chote hicho na nyinyi kama ndio wizara na ndio dhamana, mlichukua hatua gani kama wizara kuomba radhi bila kupitia humu kwenye swali hii. Mlichukua hatua gani kama wizara, ikiwa wewe waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wako, kwenda kule kuwaomba radhi walimu, wanafunzi na wazee wa skuli hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kwenda kama kwenda hatujenda kuomba radhi. Kwamba kama katoka waziri au Naibu Waziri au Katibu Mkuu kwenda katika hii skuli kuomba radhi. Lakini tuliwaandikia barua rasmi ya wizara kwa kuwaomba radhi kwa tokeo ambalo lilifanyika bila ya kukusudiwa.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kati ya skuli zilizofanya mitihani ni skuli zipi zimefanya vizuri kati ya skuli za serikali na skuli za binafsi. Pia, ni skuli gani ya mwanzo na ya mwisho katika mitihani ya Kidato cha Pili, kwa mwaka 2014.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, skuli ambazo zilifanya vizuri zaidi kati ya skuli za serikali na skuli za binafsi. Skuli zetu za serikali ziliongoza kufanya vizuri.

Skuli ya kwanza iliyopata nafasi ya kwanza ni Skuli ya Lumumba na skuli ambayo ilipata nafasi ya mwisho kabisa ni skuli ya Chokocho Pemba. *(Makofi)*

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nikaweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali moja dogo la nyongeza. Mhe Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri, kwa kukiri kwamba walilofanya ni kosa, na katika kukiri huko wakajaribu kuiandikia skuli hiyo barua.

Lakini Mhe. Spika, ninavyofahamu mimi ni kwamba kutokana na tatizo lilivyokuwa ni kubwa, mpaka skuli ikaiandikia barua wizara, na wizara ikajitosheleza kwa barua yake. Je, hawaoni kwamba hatua hiyo waliyoifanya wamezidi kuwavunja moyo walimu na wazee wa skuli hiyo, na ni lini wizara

itafuatilia kutokana na kadhia hiyo waliyoipata walimu na wanafunzi wa skuli hiyo. Ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kama jibu langu mama ambavyo nililizungumza, tulikiri kama ni kweli wizara ilifanya makosa na kwa kweli Mhe. Spika, hakuna mkamilifu katika hili. Wizara tuna umakini mkubwa na watendaji wangu wanafanyakazi zao kwa umakini mkubwa. Lakini aliyekamilika ni Mwenyezi Mungu tu, na ndio maana umakini wetu wote suala hili likatokea.

Mhe. Spika, kama ambavyo nilisema kama wizara baada ya kulitambua hilo iliwaandikia skuli hii na kuomba radhi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kama Wawakilishi wako wanatushauri ni bora twende ana kwa ana kwa walimu na wazazi. Hilo Mhe. Spika, sio tatizo na ninaahidi hapa kama nitafuatilia mimi mwenyewe ama Naibu Waziri tutakwenda katika skuli hii na kukaa pamoja, walimu na wazazi ili kutulimalize. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2015/2016
### Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kama tulivyokubaliana jana, kwamba leo mara baada ya kipindi cha maswali tumkaribishe Mhe. Waziri ili atufanyie majumuisho na tumalize kazi hii kwa kipindi hiki cha asubuhi, ya hoja hii ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Kwanza nichukuwe nafasi kuwaomba wanadhimu wetu waendelee kuwahimiza Waheshimiwa Wajumbe, walioko nje waingie bado tuna upungufu mdogo, lakini ni vyema tukawa wengi zaidi ili tukaipitisha hoja hii kwa nguvu kubwa zaidi. Baada ya hayo basi sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhanahu Wataallah,* kwa kunipa uwezo wa kusimama hapa ili niweze kufanya majumuisho ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, napenda kukushukuru wewe binafsi na kuwashukuru Waheshmiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, waliochangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, moja kwa moja, sikupata waliochangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, michango yao kwa njia moja au nyengine itaweza kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya wizara. Miongoni mwa wajumbe waliochangia katika hotuba ya bajeti ya wizara ni pamoja na:

1. Mhe. Hassan Hamad Omar
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Hamza Hassan Juma
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
5. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
6. Mhe. Kazija Khamis Kona
7. Mhe. Mgeni Hassan Juma
8. Mhe. Mwanaid Kassim Mussa
9. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
10 Mhe. Farida Amour Mohammed
11. Mhe. Fatma Mbarouk Said
12. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
13. Mhe. Abdi Mosi Kombo
14. Mhe. Marina Joel Thomas
15. Mhe. Nassor Salim Ali
16. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
17. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
18. Mhe. Jaku Mohammed Ayoub na
19 Mhe. Amina Iddi Mabrouk

**Mhe. Spika:** Mhe. Jaku, anaitwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Samahani Mhe. Spika, na naomba radhi kwa Mhe. Mjumbe.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kuzungumzia suala la wazee. Hili nimelipa nafasi ya kwanza kabisa. Mhe. Spika, wapo wajumbe wengi waliochangia juu ya suala muhimu la kuwahudumia wazee wetu. Lakini zaidi wamepongeza juu ya suala zima la kuwapatia pencheni wazee wote wanaoanzia umri wa miaka 70, na wengine wakasema hata wa miaka 60 kama hali zao ni mbaya basi wasaidiwe na kuendelea.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Shadya Mohammed, Mhe. Farida Amour, Mhe. Mwanaidi Kassim, Mhe. Hussein Ibrahim, Mhe. Nassor Salim na Mhe. Mohammed, kwa michango yao na pongezi kwa wizara juu ya suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, imeandaa Sera ya Hifadhi ya Jamii, ambayo pamoja na mambo mengine imeelekeza suala la kuwahudumia wazee, ikiwemo kuwapatia pensheni kwa kuzingatia Sera za CCM za mwaka 2010/2015 na maelekezo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, aliyoyatoa katika Baraza la Wawakilishi la mwanzo, ndio ikaandaa sera hiyo.

Mhe. Spika, zoezi la kuwatambua wazee wanaostahiki kupatiwa pensheni linaendelea Unguja na Pemba. Baada ya zoezi hilo wazee wote watakaotambuliwa watapatiwa vitambulisho maalum, kwa kupatiwa huduma mbali mbali, ikiwemo usafiri, matibabu na pensheni yao. Ulipaji wa pensheni utasimamiwa na wizara yenyewe ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, hapana atakayekosa, walemavu wote nao watapata pensheni.

Mhe. Spika, hizo zote ni jitihada zinazotokana na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, kwa niaba ya serikali ili kutekeleza azma ya malengo matukufu ya Mapinduzi ya mwaka 1964 ya kuwahudumia wazee wa Zanzibar na kuwapatia maisha bora.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mohammed Mbwana, kuwa vigezo vilivyotumika kujua umri halisi wa wazee ni pamoja na kuangalia vitambulisho vyao vya Mzanzibari Mkaazi, pasi ya uraia, vyeti vya kuzaliwa, matukio ya historia, uthibitisho wa kuingia kazini kwa wale waajiriwa, ndugu wa karibu pamoja na uongozi wa Sheha, wote wanashirikishwa hao.

Mhe. Spika, napenda kumshukuru Mhe. Hassan Hamad Omar, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kwa hotuba yao nzuri iliyoipongeza wizara. Tunamuahidi kuwa michango yao na maelekezo yao ya kuimarisha utendaji tutayafanyia kazi ili kuimarisha ufanisi wa kiutekelezaji.

Mhe. Spika, napenda kuwaarifu Mhe. Hassan na Mhe. Mohammed Mbwana kuwa ujenzi wa jengo la Wizara Pemba kwa hivi sasa unasimamiwa na Wizara ya Fedha, ambapo tayari wameshatangaza zabuni ya ujenzi huo tarehe 25 Mei, 2015; zabuni Nam: MOF/W/ICB/02/2014/2015.

Mhe. Spika, Napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kuwa ni kweli nyumba ya Limbani inahitaji matengenezo na katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara iliomba fedha kwa ajili ya ukarabati wa jengo hilo na inategemewa kuingiziwa fedha hizo hivi karibuni kwa ajili ya matengenezo hayo. Mhe. Jaku, tutajitahidi ili wazee wa Limbani nao wajisikie wako kwao.

Mhe. Spika, nashukuru kwa ushauri uliotolewa na Mhe. Hassan Hamad Omar, kuhusu kuwapatia mafunzo watendaji wa Idara ya Ushirika. Ushauri umepokelewa wa kuwapatia mafunzo watendaji wa Idara. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara imepanga kuwapatia mafunzo ya muda mfupi watendaji 25 wa Idara ya Ushirika kwenye maeneo ya uongozi na uendeshaji wa vyama vya ushirika na watendaji 10 kwenye maeneo ya usimamizi na ukaguzi wa hesabu za vyama vya ushirika. Katika hao Mhe. spika, wanawake watakuwa 15 na wanaume watakuwa 10, hapo *gender* tumeiangalia.

Pia, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni wadau, kwa bahati mbaya Waziri wa Uvuvi hayupo, ni wadau muhimu sana na tulifanya nao kazi kwa pamoja hadi kufanikisha kupatikana kwa boti za kubebea mwani. Aidha, wamo katika Kamati ya Uwezeshaji ya kisekta na Kamati ya kitaalamu.

**Suala la Uzalilishaji Wanawake na Watoto**

Mhe. Spika, napenda kuwajibu Mheshimiwa Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Viwe Khamis Abdalla na Mhe. Wanu Hafidh Ameir, kuwa Wizara inaratibu shughuli za kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Hata hivyo, suala hili ni mtambuka linagusa taasisi nyingi kila moja ikiwa na jukumu lake. Jukumu la ununuzi wa mashine ya *DNA* linashughulikiwa na Wizara ya Afya na Wizara ya Katiba na Sheria. Aidha, Balozi wa Jumuiya ya Umoja wa Ulaya ameahidi kusaidia ununuzi wa mashine hiyo. Mashine hiyo itakapopatikana imependekezwa iwekwe katika Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Kwa hivyo, mashine inakuja wanaojificha kwa sababu hakuna mashine Mwenyezi Mungu atawafichua.

Mhe. Spika, kuhusu nyumba salama ni kweli inashughulikia watoto pamoja na wanawake wanaopata matatizo mbali mbali ya ukatili na udhalilishaji kwa kuwapatiwa hifadhi katika nyumba hiyo pamoja na kufuatilia kesi zao Mahakamani na Vituo vya Polisi.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri, samahani sana kukukatisha lakini nilikuwa naombi Waheshimiwa Wajumbe, tumsikilize Mhe. Waziri, anatoa majumuisho hasa hasa

Mhe. Jaku na Mhe. Gavu, maana hapo soga imezidi, sasa inaondoa nidhamu, aa, bora kaondoka. *(Makofi)*

Mhe. Waziri, sasa endelea naona utulivu sasa upo.

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, kuhusu nyumba salama ni kweli inashughulikia watoto pamoja na wanawake wanaopata matatizo mbali mbali ya ukatili na udhalilishaji kwa kuwapatiwa hifadhi katika nyumba hiyo pamoja na kufuatilia kesi zao Mahakamani na Vituo vya Polisi. Uendeshaji wa nyumba hiyo ni kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011, ambayo inaelezea watoto wote waliopatwa na kadhia ya udhalilishaji wawekwe nyumba salama na kuna watu maalum walioajiriwa kwa kusimamia ili wapate huduma mbali mbali watoto hawa na wapewe ushauri nasaha na pia kufuatilia kesi zao Mahakamani.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mshimba, kuhusu suala la *DPP* na Polisi Jamii, tuna ushirikiano wa karibu na tunafanya nao kazi kwa pamoja. Hata hivyo, ushauri wake tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika kuwa suala la udhalilishaji wa kijinsia huchangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la talaka, kwa kuelewa hili Wizara imefanya Utafiti na kugundua kwamba, miongoni mwa sababu zilizojitokeza ni migongano ya ndoa, udhalilishaji wa majumbani, kukosa uaminifu, kutokuwa na matunzo kwa watoto, kutelekeza familia na kukosa taaluma ya ndoa kwa wanandoa. Wizara inalifanyia kazi suala hili kwa kushirikiana na viongozi wa dini na jamii kwa ujumla.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Shadya, kwamba kuwa, Wizara inafuatilia kwa karibu kesi za udhalilishaji lakini bado hali ni ngumu na inakatisha tamaa kwamba kesi nyingi zinachukua muda mrefu kusikilizwa na kutolewa maamuzi yanayostahiki. Aidha, suala la kutoa ushahidi limekuwa ni changamoto kubwa, watu wanapoitwa kwenda kutoa ushahidi hawapatikani wanaona muhali, fulani mimi nikimkalia ushahidi itakuwaje, sasa mambo haya ndio yanayoturudisha nyuma, lakini sisi Wizara tunafuatilia.

Mhe. Spika, kuhusu vijana apenda Kuwajibu Mhe. Wanu, Mhe. Farida, Mhe. Nassor na Mhe. Viwe, kuwa mchakato wa uanzishaji wa Baraza la Vijana unaendelea kwa kuwahamasisha vijana kujiorodhesha katika Shehia zao. Uundaji wa Mabaraza hayo unaanza katika ngazi ya Shehia, kwani wajumbe wa mabaraza ya Wilaya wanatoka kwenye Shehia na wa Taifa wanatoka kwenye Wilaya. Aidha, napenda kuwatoa wasi wasi Waheshimiwa wajumbe kuwa, Baraza hilo litafanya

kazi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizowekwa bila ya ubaguzi wowote hakuna CUF, hakuna CCM, sisi tunachoangalia ni uundwaji wa Baraza la vijana.

**Vikundi vya Wanawake vya Kiuchumi**

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Wanu Hafidh, kuwa vikundi 50 vya wanawake vitakavyoundwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni vipya, lakini bado tunaendelea kuviendeleza vya zamani kwa kuwapa mikopo na taaluma ya kuendeleza vikundi vyao, zaidi nimwambie kwamba kuna vikundi vyengine vinakuwa havijui utaratibu, kwa hivyo, tunawasomesha wao ili na wao wapate kuwaelimisha wenziwao, ili vikundi viweze kuongezeka zaidi.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, kuwa anasema vitabu vile kila siku vinaandikwa uratibu, utaribu, maana yake nini, mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu uratibu tu. Nataka nimwambie Mheshimiwa, kwamba sisi hiyo ndio kazi yetu maalum Wizara ya Uwezeshaji, shughuli zote za Vijana lazima tuziratibu, wanawake lazima turatibu, wazee na watoto lazima turatibu, zinazofanywa na taasisi mbali mbali na sisi wenyewe. Hiyo ndio kazi yetu, kwa hivyo vitabu vyetu vyote utaviona na suala la uratibu, usihangaike wala usishughulike ndio kazi yetu hiyo.

**Benki ya Wanawake**

Mhe. Spika, napenda kuwajibu Mhe. Mshimba, Mhe. Wanu, Mhe. Hamza, Mhe. Shadya, Mhe. Farida, Mhe. Amina Iddi, Mhe. Mwanaidi na Mhe. Viwe, kuhusu uanzishaji wa Benki ya Wanawake, wao wamesikitika, kwa nini hadi leo hatujaanzisha benki ya wanawake. Nataka niwaambie wanawake benki ya wanawake ipo, lakini kwa sababu ya uchache wa fedha tumekubaliana kwamba sasa Benki ya wanawake ifunguliwe katika dirisha ambalo litapitia benki ya watu wa Zaznibar, Benki ya watu wa Zanzibar itakuwa na diridha maalum kwa ajili ya wanawake tu na hilo dirisha msije mkasema ni dirisha dogo hivi na hivi, itakuwa dirisha rasmi; wanawake wakifika pale watajua wapi tunahudumiwa. Kwa hivyo, tunaomba mtuunge mkono na suala hili ili liweze kufanikiwa, dua zenu tunataka kwa ujumla.

Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Hamza Hassan Juma, kuwa wale wote walioomba mikopo na wakakamilisha taratibu, watapatiwa mikopo hiyo hatua kwa hatua. Mimi mwenyewe nitahakikisha kwamba nafuatilia na ndio kazi yangu kufuatilia na kuona kwamba wanawake zaidi wanapatiwa mikopo, vijana nao wanapatiwa mikopo, wazee nao wenye nguvu zao wanaweza kupatiwa mikopo.

Lakini nataka niwaambie jambo moja Waheshimiwa, mujue, vijana mimi uwezo wa kuwaajiri sinao, anayeajiri ni Mhe. Harouna, lakini vijana wengine wana ila hawataki kujituma, jembe hawalitaki, hawataki kujituma kwa sababu hata vikundi vya ushirika kama hujitumi vinaweza vikafa hivi hivi, kwa hivyo, natoa wito kwa vijana wasikae nje wakalalamika Wizara yao ipo na Mhe. Mahamoud, pale yupo nataka tuungane kwa pamoja ili tuwaeleweshe vijana nini wafanye ili mujikwamue na hali ngumu ya uchumi.

Mhe. Spika, Mhe. Viwe, ametaka kujua sababu za kuongezeka marejesho ya mikopo. Sababu hizo ni uanzishwaji wa vikundi imara, uelewa wa walengwa wa mikopo, umakini katika kuidhinisha viwango vya mikopo na ufuatiliaji wa karibu wa mikopo, tunapomkopesha mtu tayari tumeshamkagua; ana sifa zote za kupewa mikopo tukimpatia mkopo mwezi wa kwanza wa pili tunakwenda hodi tunaangalia kazi zao, kweli hawa wanaifanyia kazi hii mikopo na tunaweza kuanzia hapo tukaanza kuchukua kidogo kidogo michango watakayotupa. Ndio sababu hasa kwamba sasa mikopo inarejeshwa tena vizuri sana tunashukuru Mungu.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Kazija Khamis, kuwa vijana watakaounganishwa na fursa za mikopo ni wale waliotayari, wenye shughuli na watakaotimiza masharti, kama mtu hana shughuli yoyote kakaa anasubiri Serikali imuajiri, hana mpango wowote kwa kweli itakuwa ni tatizo kumpa mkopo. Lakini kwa wale watakaotimiza sifa tukawakagua tukawaona kweli wanajituma nakuhakikishieni kwamba watapata mikopo.

Mhe. Spika, Mhe. Mwanaidi na Mhe. Marina, wanataka kuelewa sababu za mikopo iliyotolewa kuwa ni michache lakini fedha zilizotolewa ni nyingi. Hii inatokana na kuwa hivi sasa viwango vya mikopo vinavyoombwa ni vikubwa na wajasiriamali wetu wamejikita zaidi katika shughuli za uzalishaji ambazo zinahitaji ununuzi wa vitendea kazi ambavyo vina thamani kubwa, na sisi mkopo wetu mwisho wetu ni milioni tano, sasa watu wanataka mashine za nini, wanataka mambo gani, kwa hivyo, inakuwa ni tatizo kidogo.

Mhe. Spika, Kuhusu suala la Mhe. Amina Iddi Mabrouk, juu ya asilimia ya urejeshaji wa mikopo, napenda kumjibu kuwa fedha zilizotolewa zipo katika kiambatisho Nam. 2 ambazo ni shilingi milioni mia nane sabini na tisa laki tatu elfu arobaini na mbili. Asilimia ya urejeshaji ni 96 ya matarajio ya fedha zilizopangwa kurejeshwa katika kipindi hicho.

Mhe. Spika, Mhe. Jaku, anaeleza kuwa fedha za Mfuko uliokuwa wa AK/JK zilizolipwa ni kidogo ikilinganishwa na zilizokopeshwa. Mhe. Jaku, nakuomba nikwambie hivi aidha kuwa fedha za mikopo wanazopewa wateja wa mikopo ni kidogo mno ukilinganisha na mahitaji ya biashara. Mimi kwanza sikubaliani na

maelezo yako Mhe. Jaku, kwamba mfuko wa AK/JK fedha zake zilikuwa hazirejeshwi ipasavyo na wateja waliokopeshwa. Wizara ya Uwezeshaji Ustawi wa Jamii Vijana Wanawake na Watoto ndio uliofufua ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo na ikaweza kukusanya na ikafikia kiwango hicho, tunamuomba Mhe. Jaku, awahimize wapiga kura wake wa Jimbo la Muyuni ambao ni wadaiwa sugu wanadaiwa pesa nyingi, warejeshe pesa za mikopo walizopewa ili na wengine wapate kunufaika na fedha hizo kwani hizi si fedha za sadaka. Kuhusu pesa wanazokopeshwa Wajasiriamali ni kwa mujibu wa mahitaji yao kulingana na biashara zao zinatosha, aidha, kabla ya kuwapa mikopo biashara zao zinafanyiwa uchambuzi yakinifu na kukubaliana juu ya gharama za biashara hizo.

Kusema kweli sawabu Mfuko wa JK/AK watu walikuwa hawafuatili kabisa malipo haya, sisi tulipoingia hapa mwaka huu tukasema hatukubali lazima tufuatilie, tumefuatilia ndio tukapata hichi tulichokipata, kwa hivyo, jamani nyinyi mko kwenye Majimbo yenu huko, sio Mhe. Jaku, tu lakini yeyote aliyekuwa na watu wake hawajalipa walipe, hatukubali walipe walipe walipe.(*Makofi*)

**Sheria Katika kukabiliana na kesi za udhalilishaji**

Mhe. Spika, naomba kuwajibu Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Moh’d Mbwana na Mhe. Amina Iddi, waliosisitiza suala la marekebisho na usimamizi wa sheria kwa kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto, kuwa suala hili limo katika mpango wa mageuzi ya Mfumo wa Sheria ya Mtoto na katika Mpango wa miaka mitano wa kupambana na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Zoezi la kuifanyia marekebisho Sheria ya Ushahidi limeanza na linaratibiwa na Tume ya Kurekebisha Sheria. Lakini tuna tatizo kubwa mjomba anambaka mtoto wa ndugu yake, baba anambaka mtoto wake, kaka anambaka ndugu yake, jamani tujitahidini vibaya hivyo tusifanye. (*Makofi*)

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Shadya, kwamba Wizara ina mashirikiano ya karibu na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ikiwa ni pamoja na kuendesha kituo cha kulea na kukuza wajasiriamali kilichopo Chuo cha Karume Mbweni. Hata hivyo, tumepokea ushauri wake na mashirikiano hayo yataendelea baadae na suala hili baadae litakwenda na Pemba, kila tunapofanya shughuli yetu Unguja na baadae tunaipeleka Pemba hatukubali kwa sababu tunajua Serikali ya Zanzibar ni Unguja pamoja na Pemba.

**Suala la kutelekeza Watoto**

Mhe. Spika, Wizara inachukua jitihada ya kuwaita wazee wanaotelekeza watoto na wasiotoa matunzo na kuzungumza nao pamoja kuwakumbusha wajibu wao juu ya

malezi na matunzo. Pamoja na hayo, huwa tunaweka makubaliano baina ya pande mbili ili kutoa matunzo kwa watoto.

**Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

Mhe. Spika, napenda kumjuilisha Mhe. Shadya na Mhe. Muhammed Mbwana pamoja na wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa, Wizara ina mpango wa kuanzisha kituo cha kukuza wajasiriamali kwa upande wa Pemba. Aidha, Wizara imeanza kuzungumza na Washirika wa Maendeleo ili kusaidia katika hili. Lakini pia nataka niseme kwamba Mhe. Spika, sisi tutafungua chuo cha Kibokwa cha kutengeneza mambo ya *solar*. Kile ni Chuo, lakini Chuo kile kinapokea walimu kutoka Vijijini na wanafunzi wanaosomeshwa kutoka vijijini, wao ndio wanye matatizo kwamba hawezi kununua umeme huu wa kawaida. Kwa hivyo, tunataka wapate umeme ule wa jua. Sasa tuliwapeleka India Wapemba wamo, Waunguja wamo, hata Kisiwa Penza yumo mwanamke hodari kama nini, tunae pale chuwoni.

Mhe. Spika, Mhe. Nassor Salim (Aljazira) na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, walitaka kujua serikali ina mpango gani wa kuwawezesha vijana wakiwemo wanaomaliza vyuo vikuu na wenye biashara ndogo ndogo wawezeshwe ili kujiajiri.

Wizara inao mpango huo wa kuwawezesha kwa kuwapa taaluma ya ujasiriamali na kuwaunganisha na huduma za mikopo. Aidha, kituo cha kulelea wajasiriamali kilichopo Mbweni kinafundisha vijana wakiwemo waliomaliza vyuo vya elimu ya juu na baadhi ya vijana waliojiunga na kituo hicho tayari wameanzisha makampuni katika fani zao na wanajipatia kipato.

Mhe. Spika, Mhe. Moh’d Mbwana Hamad, aliuliza kuhusu waliopatiwa mafunzo ya uwezeshaji. Lengo lilikua ni kutoa mafunzo katika awamu nne (4), lakini kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha yametolewa awamu moja (1) tu kwa vijana 71. Hiyo ni kwa sababu ya pesa, kwa hivyo, mwenzangu utusamehe ndio mwambo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuhusu chuo cha kufundisha wanawake (*Barefoot Collage)* kitachukua wanawake kumi na mbili (12) kwa kila awamu na watapatiwa mafunzo kwa muda wa miezi sita. Katika kuchagua wanafunzi wa kujiunga katika chuo hicho, mkazo unaelekezwa kwa wanawake kutoka katika maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma ya umeme Unguja na Pemba.

**Ushirika**

Mhe. Spika, kuhusu jengo la Idara ya Ushirika, napenda kumjibu Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na Mhe. Marina Joel Thomas, kwamba wizara imeanza kufanya

matengenezo ya jengo katika eneo la Migombani ambapo baadae Idara hiyo itahamia. Matengenezo hayo, yamefikia asilimia 70.

Mhe. Spika, napenda kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa michango na pongezi mlizotupa katika utekelezaji wa kazi zetu. Napenda kuahidi kuwa maoni na ushauri wenu wote mliotupa tutaufanyia kazi ili kuongeza ufanisi wa majukumu yetu ya kila siku kwa manufaa ya maendeleo ya wanawake, vijana, wazee, watoto na jamii kwa ujumla. Baada ya maelezo hayo kama kuna mtu niliyomkosea naomba radhi sana anisamehe. Mhe. Spika sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri, tunakushukuru na sasa Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi kuwashukuru sana tupo idadi ya kutosha niwahoji basi wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hii ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, kwa mwaka 2015/16 wanyanyue mikono. Wanaokataa, wote wamekubali, kwa hiyo, wamekubali wameshinda.

*(Hoja imetolewa imeamuliwa)*

*(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, sasa naomba Baraza lako Tukufu likae Kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha Vifungu vya Matumizi vya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**Fungu Q(01) - Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 07 | Idara ya Ushirika | Sh. 17,606,000/= |
| **Jumla Kuu ya Fungu** | | **Sh. 17,606,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu Q(01) - Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu P(01) | Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | |
| Kifungu S(01) | Programu ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Mikopo ya Uwezeshaji | Sh. 72,509,000/= |

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni ndogo tu. Hapa Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, alipokuwa akitaja kataja wadaiwa sugu wananchi wa Jimbo la Muyuni na mimi kama kiongozi wao nitakuwa sijafanya haki ya kupata kujua. Kwa mujibu wa kitabu chake cha taarifa za waliokuwa na Mfuko wa JK na AK hadi 2000, Kusini ni milioni arubaini na moja laki, tatu, thalathini na tatu, pesa zilizorudishwa ni milioni tatu. Kusini kuna Wilaya mbili, nataka anambie tu Jimbo la Muyuni ni shilingi ngapi wanaodaiwa, isijekuwa ni milioni moja au milioni mbili, apate kunipa taarifa hiyo nipate kujua nikakae na wananchi wangu.

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na nampongeza sana Mhe. Jaku, ikiwa watu wake wamesharejesha mikopo basi pongezi zote ziende kwako na kwa watu wako. Kwa sababu Mheshimiwa, tatizo kubwa ni kuwa watu hawajarejesha mikopo, leo anakubali mwenyewe kama watu wamerejesha. Kwa hivyo na mimi nakubali kwamba watu wamerejesha, hongera sana.

**Mhe. Spika:** Nafikiri suala lako halijajibika, labda suala lako unasema halijajibika.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Nafikiri Mhe. Waziri, hakunikisia labda nizungumze kidogo kidogo, na anamchezo wa kusungumza haraka haraka sana, naomba anisikilize.

Hapa Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, alipokuwa akitaja alisema kwamba katika wadaiwa sugu ni wananchi wa Jimbo la Muyuni. Ikiwa mimi ni kiongozi wao na ni Mwakilishi wao natakakujua hizi pesa kwa mujibu wa taarifa ya kitabu chako Kusini kuna Wilaya mbili na tuna majimbo manne kuna Chwaka la Mhe. Issa Gavu, Uzini Mhe. Muhammedraza, Muyuni ambalo naongoza mimi na Makunduzi Mhe. Haroun Suleiman.

Sasa nataka kujua wananchi wa Jimbo la Munyuni katika hizi sijafanya ni shilingi ngapi wanazodaiwa, isijekuwa ni milioni moja au milioni mbili na nusu, nijue nini cha kukifanya tupate kujua ukweli wake Mhe. Waziri.

**Mhe. Spika:** Inavyoelekea Mhe. Waziri, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni anataka kusaidia ili warejeshe, kwa hivyo, anauliza ni kiasi gani.

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe Mwenyekiti, nashukuru tena na nataka nimwambie Mhe. Jaku Hashim Ayoub, anisaidie Watu wa Muyuni wanadaiwa shilingi milioni 5. (*Makofi*)

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Namshukuru sana Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, kunambia wananchi wa Jimbo la Muyuni, naomba tukae mimi na wananchi wangu, tupate ukweli huu na kama pana ukweli huo niko tayari kuchukua mzigo huu. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Hao ndio baadhi ya Wawakilishi Makini. Tunaendelea.

**Jumla ya Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Mikopo ya Uwezeshaji** **Sh. 72,509,000/=**

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu S(02) | ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika | Sh. 41,520,000/= |
| Kifungu S(03) | Uratibu na Uendeshaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | Sh. 555,747,000/= |
| | **Jumla Kuu ya Kifungu** | **Sh. 669,776,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu S(02) | Usimamizi wa Huduma ya Utawala na Utumishi | Sh. 2,182,700,000/= |
| Kifungu S(03) | Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba | Sh. 768,864,000/= |
| Kifungu P(04) | Programu ya Uongozi na Mipango ya Uzeshaji na Ustawi wa Jamii | Sh. 337,534,000/= |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Kifungu P(02) - Programu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji Wanawake**

Kifungu S(01) Programu Ndogo ya Uratibu wa Masuala jinsia na Maendelea ya Wanawake Sh. 276,374,000/=

Kifungu S(02) Programu Ndogo ya Mapambano ya Udhalilishaji Dhidi ya Wanawake na Watoto Sh. 24,245,000/=

Kifungu P(20) Programu ya Kuimarisha Hifadhi ya Jamii

Kifungu S(01) Programu Ndogo ya Uratibu wa Huduma za Uhifadhi

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, hetu tunarudia kidogo kwa sababu ile jumla ya programu hakuwahi kuisoma tuone kama nayo mnaikubali.

Jumla ya Programu P(02) ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji wa Wanawake ni Sh. 3,619,000/=

Kifungu P(03) Programu ya Kuimarisha Hifadhi ya Jamii

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri, kwa kukiri nyumba ya Wazee Limbani hali yake hairidhishi na kukiri kuwa ataifanyia matengenezo. Hilo nimshukuru lakini nimuombe tu matengenezo yake ni ya haraka kutokana na hali yenyewe. Kwa wakati huo nilipokuwepo katika Kamati hiyo hali tumeiona na Mhe. Makamu Mwenyekiti wangu wakati huo ni Mhe. Hija Hassan Hija.

Hoja yangu sasa hivi ipo katika nyumba ya Mazizini, ipo katika hali nzuri ilivyotengenezwa, lakini hivi sasa hali yake hairidhishi na pesa anazopewa milioni nne laki tano kwa kweli ni kidogo sana, ile nyumba ya kileo na ni nyumba *standard* kabisa. Hivi sasa kuna mpira wa kuchotea maji kunako kisima wote umetoboka umefungiwa mpira wa baskeli, nyumba inavuja. Je, Mhe. Waziri, unatoa kauli gani ambapo hapana gharama kubwa hata hivyo kwa muda huu na haina bajeti ya kutengeneza nyumba ile.

Kuna msema wanaosema Waswahili; "Usipoziba ufa utajenga ukuta". Ile nyuma hivi sasa imeshaanza kuleta wasi wasi.

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri tulivyokuwa tunapeana mikataba ya

ile nyumba huyu aliyejenga nyumba ndiyo aliyekubali kwamba kukitokea tatizo lolote kuhusu nyumba atatengeneza yeye. Kwa hivyo na sisi tayari tumesharipoti juu ya suala hili. Sasa tutaendelea kumkumbusha kwamba hali isijeikawa mbaya zaidi, lakini hilo tunalijua na tumeshaanza kulifanyia kazi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri, kwa majibu yake, lakini kilichohitajika hivi sasa ni pesa ndogo sana. Kwa nilivyoiyona mimi hali ilivyo kama milioni mbili, kumsubiri aliyejenga ile nyumba hatumjui yupo wapi, lini atakuja, wapi atapatikana, mmeshakwenda kuripoti kwa muda urefu Mhe. Waziri. Hili ninalolizungumza mimi nimelifuatilia, nimekwenda kuripoti, lakini tushukuru kutujengea nyumba kama ile ya thamani ya bilioni sio jambo dogo.

Kuna msemo Waswahili wanasema; "Shika shika na mwenyewe uko nyuma". Sasa hebu tueleze kitu kama milioni mbili Mhe. Waziri, ni pesa ndogo Mhe. Waziri. Hili nikuombe mama yangu ulikubali ulichukue jukumu hili ili kesho ikafanyike kazi. Maji yanamwagika vibaya sana, ni sadaka kubwa.

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Kwanza Mhe. Mwenyekiti, naomba nimwambie Mhe. Jaku Hashim Ayoub, hivi, mambo mbali mbali, matatizo mbali mbali katika ile nyumba yanatokea, tunayafanyia kazi sisi Wizara ya Uwezeshaji. Kwa shilingi milioni mbili, mpaka tatu mpaka nne, Katibu Mkuu shahidi yule pale, tunazito sisi kushughulikia ile nyumba. Kwa hivyo, sasa yale mambo makubwa ndiyo tunamuachia mwenzetu kwa sababu sisi hatuna vifungu vya hivyo zaidi.

Kwa hivyo, tutalihimiza jambo hili ili lifanyike tusije tukaharibikiwa.

Kifungu S(01) Programu Ndogo ya Uratibu wa Huduma za Uhifadhi,

Sh. 2,624,505,000/=

Kifigungu S(02) Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana
Sh. 382,666,000/=

**Jumla ya Programu Kuu ya P(03)**
**Sh. 3,7171000/=**

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Kifungu P(04)** | **Programu ya Uongozi na Mipango ya Uwezeshaji na Ustawi wa Jamii** | | |
| Kifungu S(01) | Programu Ndogo ya Kusimamia Mipango, Sera na Tafiti za Wizara | Sh. | 85,970,000/= |
| Kifungu S(02) | Programu Ndogo ya Usimamizi wa Huduma za Utawala na Utumishi | Sh. | 2,182,700,000/= |
| Kifungu S(03) | Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba | Sh. | 768,864,000/= |

Jumla ya Kifungu P(04) Programu ya Uwongozi na Mipango ya Uwezesaji na Ustawi wa Jamii, **Sh. 337,534,000/=**

Jumla Kuu ya Programu zote nne ipo ukurasa wa ni **Sh. 715,100,000/=**

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, ilikuvyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawakae na Watoto bila ya mabadiliko sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza iliyakubali makadirio hayo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Naafiki.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji basi wale wanaokubaliana na Makadirio hayo wanyanyue mikono, wale wanaokataa, waliokubali wote wameshinda.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, upo? Muda upo.

Waheshimiwa Wajumbe, nachukua nafasi hii kuwashukuru sana kwa kupitisha hoja hii ambayo bahati nzuri sikuona mkono wowote unaokataa hoja yenyewe na unaokataa makadirio haya. Wajumbe wote waliohudhuria tena kwa wingi leo,

nashukuru wote wamekubali. Kwa hivyo, nakushukuruni sana kwa kazi hiyo nzuri. Lakini namshukuru zaidi Mhe. Waziri na Watendaji wake wote.

Waheshimiwa Wajumbe, tuna kitabu kinene kidogo, lakini kipo mpaka *page* 78, mwenye hoja hii alinambia atatumia muda kama wa saa 1:40 au 45. Muda uliopo ni saa 1:35, si bora tumuongezee dakika tano baadae amalize.

*(Wajumbe wote wamekaa kwa kupiga makelele)*

Kama hamtaki basi bwana.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, hii ni dalili nzuri kwamba ikiwa tutakuwa tunahudhuria kwa wingi kama hivi na kwa sababu ya furaha hii ya kuhudhuria kwa wingi nategemea jioni Wizara hii muhimu sana ya Elimu itakapowasilishwa tutakuwa na wingi kama huu. (*Makofi*)

Kwa kuwa muda uliopo hautamtosha Mhe. Waziri, kuwasilisha hotuba yenye kurasa kama 75, basi tusitishe shughuli zetu. Naelewa kwamba kuna wengine wameshapangiwa kutoa hotuba katika misikiti mbali mbali. Kwa hivyo, tusitishe shughuli zetu na turudi tena hapo saa 11:00 jioni. Kwa maana hiyo basi naakhirisha Kikao hichi hadi saa 11:00 jioni leo tufike mapema.

*(Saa 11:42 mchana Kikao kiliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** *Bismillahi Rahmani Rahiim,* Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa liingie katika Kamati ili niweze kutoa maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2015/16.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, muumba ardhi na mbingu na kutuwezesha kukutana tena katika kikao cha Bajeti cha Baraza hili tukiwa wazima wenye afya njema, na namuomba aniwezeshe kuiwasilisha hotuba hii vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, tumebakisha siku kumi na tatu kufika mwezi wa Ramadhani Mwenyezi Mungu atupe afya na uzima kuukaribisha mwezi huu na kuidiriki funga ya mwezi wa Ramadhani, na atupe futari ya halali na kutulipa malipo mema kesho akhera amin. Mhe. Mwenyekiti, hiki ni kikao cha tano cha bajeti tangu kuingia madarakani kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa alivyokuwa karibu sana na Wizara yangu kwa kutupa miongozo na maelekezo ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kuiendeleza sekta ya elimu. Vile vile, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Maalim Seif Sharrif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa michango yao na mashauriano yao na Mhe. Rais wetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nawe upokee pongezi na shukrani zangu kwa uwezo aliokubariki Mwenyezi Mungu na kuliendesha Baraza hili kwa umakini na hekima, busara na uadilifu mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma kwa ushauri wao mzuri na miongozo waliyotupatia katika kuichambua hotuba ya bajeti ya Wizara yangu kwa undani kabisa na hekima kubwa waliyotoa.

Mhe. Mwenyekiti, pia, namshukuru kwa dhati kabisa msaidizi wangu, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Zahra Ali Hamad, kwa juhudi zake, mashirikiano yake na mimi na Wizara yetu na uadilifu wake mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Taifa letu. Aidha, napenda kuwapongeza watendaji wangu kwa kufanya kazi wote kwa pamoja wakiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, Wakurugenzi, Maafisa wa ngazi mbalimbali za elimu, wazazi, walimu na wafanyakazi wengine kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza kazi zangu. Pia, nazipongeza Taasisi zote za Elimu zinazojitegemea, Baraza la Elimu, Bodi za Elimu za Mikoa, Wilaya na Kamati za Skuli kwa utendaji wao wa kazi ambao umechangia sana katika kuleta ufanisi katika Wizara yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuishukuru kwa dhati kabisa Wizara ya Fedha kwa mashirikiano makubwa waliyotupa kwa mwaka 2014/15. Kwa ujumla, upatikanaji wa rasilimali fedha ulikuwa wa wastani kwani hadi mwishoni mwa mwezi wa Mei 2015, jumla ya Tsh 1,000,000,000/= kwa kazi za maendeleo

zilipatikana kutoka Serikalini ikiwa ni sawa na asilimia 30.3 ya makadirio ya mwaka 2014/15. Kwa upande wa kazi za kawaida, jumla ya Tsh 60,540,859,677/= zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 70.23 ya makadirio. Jadweli Namba 10(a) na 10(b) zinatoa uchambuzi zaidi. Ni matumaini yangu kwamba ushirikiano huu utaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Baraza lako Tukufu lilipata msiba wa kuondokewa na Mheshimiwa Salmin Awadh Salmin aliyekuwa Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi na Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni ambaye alifariki dunia tarehe 19/02/2015. Pia kumetokea vifo, majeruhi na uharibifu wa mali katika upepo mkali uliotokea katika Kisiwa Panza Pemba pamoja na maafa ya mvua na mafuriko yaliyotokea katika sehemu mbalimbali za nchi yetu. Baadhi ya familia ambazo nyumba zao zilibomoka au kujaa maji zimepatiwa makaazi ya muda katika skuli ya Mwanakwerekwe "C". Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi wale wote waliopoteza maisha. Pia tunawaombea wapone haraka wale wote waliojeruhiwa. Amin.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya awamu ya saba imetimiza miaka mitano. Hivyo katika hotuba yangu, naomba uniruhusu nieleze alau kwa muhutasari, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika Wizara hii kwa kipindi chote cha miaka mitano iliyopita kabla ya kuelezea utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kipindi cha mwaka 2015/16.

## MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO 2010 - 2015

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu imepata mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka mitano. Miongoni mwa mafanikio hayo kwa uchache ni haya yafuatayo:-

- Ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya lazima (maandalizi, msingi na sekondari) kutoka wanafunzi 317,278 mwaka 2010 na kufikia wanafunzi 390,464 mwaka 2015.
- Kufunguliwa kwa kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar huko Tunguu ambako kumepelekea kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kutoka wanafunzi 1,205 mwaka 2010 hadi wanafunzi 2,538 mwaka 2015. Pia, Chuo Kikuu kimeweza kupanua shughuli zake kwa kuanzisha programu za masomo mbalimbali za Shahada, Shahada ya Uzamili na Uzamivu.
- Chuo Cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa kilichokuwepo Wete, kuhamia huko Mchanga Mdogo Pemba, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kampasi mpya. Chuo hicho kitakuwa Kampasi ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kuanzia Mwezi Julai 2015.

- Kukamilika kwa ujenzi na kufanya kazi kwa skuli mpya 19 za sekondari za kisasa katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba.
- Kuongezeka kwa mashirikiano kati ya Wizara yetu na washirika mbalimbali wa maendeleo ya elimu wa ndani na nje; mfano *Global Partnership for Education (GPE), Milele Zanzibar Foundation (MZF)* na *OPEC Fund for International Development (OFID).*

## MAELEZO YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2014/15

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kueleza kwa ufupi mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 5, sasa naomba uniruhusu nieleze utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizotekelezwa katika Idara na taasisi za Wizara yangu kwa mwaka 2014/15 na matarajio na malengo ya mwaka 2015/16.

## IDARA YA SERA, MIPANGO NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Sera, Mipango na Utafiti ina majukumu ya kuandaa mipango ya maendeleo, kuratibu na kufuatilia rasilimali na misaada ya wahisani, kufanya mapitio ya tathmini ya sera, mipango na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wizara, kuratibu shughuli za utafiti wa kielimu na kusimamia ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa takwimu mbalimbali za kielimu kwa wadau.

### Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2014/15

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Wizara ilipanga kutekeleza miradi sita ya maendeleo iliyotengewa jumla ya Tsh. 26,152,450,130/=. Kati ya fedha hizo Tsh. 3,300,000,000/= za Serikali, Tsh. 9,362,128,000/= ni ruzuku kutoka kwa wahisani mbalimbali wa maendeleo na Tsh. 13,490,322,130/= ni mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Benki ya Dunia.

Hadi kufikia Mei, 2015, jumla ya Tsh. 1,000,000,000/= za Serikali zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 30.3 ya makadirio. Kwa upande wa Washirika wa Maendeleo, jumla ya Tsh. 4,884,031,899/= sawa na asilimia 21.8 ya makadirio zilipatikana. Utekelezaji halisi wa miradi ulikuwa kama ifuatavyo:-

### Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulitengewa jumla ya Tsh. 1,300,000,000/=. Kati ya hizo 100,000,000/= ni za Serikali na 1,200,000,000/= ni za *GPE* na *UNICEF*. Hadi kufikia mwezi Mei, 2015 hakuna fedha za SMZ zilizopatikana na Tsh.

56,300,400/= za wafadhili ambazo ni sawa na asilimia 4.7 zilipatikana. Maelezo zaidi ya utekelezaji wa mradi huu inapatikana katika ibara ya 14.

Mafunzo ya elimu ya maandalizi kwa walimu 350 kwa njia ya *TEHAMA* kupitia vituo vya walimu yametolewa.

i) Moduli 4 na 5 pamoja na video zake kwa ajili ya kutolea mafunzo kwa walimu wakufunzi zimeandikwa, na uandishi wa moduli ya 6 ya wenye mahitaji maalum kwa ajili ya walimu wa maandalizi unaendelea.
ii) Vifaa vya kujifunzia watoto wa Tucheze Tujifunze (TUTU) vimenunuliwa zikiwemo kadi za nambari, kadi za maneno na vibao vya kuandikia.
iii) Uandishi wa vitabu vya wanafunzi na miongozo ya walimu kwa masomo ya Kiswahili, Hisabati na Sayansi na Teknolojia unaendelea.

**Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi**

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulitengewa Tsh. 12,362,128,000/=, kati ya fedha hizo Tsh. 1,000,000,000/= ni za SMZ na Tsh. 11,362,128,000/= ni ruzuku na mkopo kutoka *Sida, UNICEF, UNESCO, GPE, OPEC Fund, Imperial College of Science and Technology* ya *UK, Milele Zanzibar Foundation* na *USAID.* Hadi kufikia mwezi Mei 2015, Tsh. 85,000,000/= za SMZ sawa na asilimia 8.5 na Tsh. 778,428,033.1/= za wahisani sawa na asilimia 35.5 ya makadirio zimepatikana. Utekelezaji wa malengo ulikuwa kama hivi ifuatavyo:- Maelezo zaidi ya utekelezaji yanapatikana katika Ibara ya 15.

i) Jumla ya madarasa 125 yamekamilishwa kati ya hayo 79 yapo Unguja na 46 Pemba.

ii) Ukarabati wa madarasa 35 ya skuli saba za Unguja na madarasa 24 katika skuli tatu za Pemba umekamilika.

iii) Jumla ya seti 3,187 za viti na meza na madawati 3,490 yamechongwa na kusambazwa katika skuli za msingi za Unguja na Pemba. Pia, Benki ya NMB imetoa msaada wa madawati 100 na kusambazwa katika Skuli za Msingi za Mwanakwerekwe “E” na Bububu “A”. Vile vile, kampuni ya Jambo plastiki imetoa msaada wa viti na meza 45 kwa Skuli ya Msingi ya Kiembesamaki “A”.

iv) Mkataba wa Mkopo wa ujenzi wa skuli 10 katika sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba umetiwa saini kati ya Serikali ya

Jamhuri ya Muungano na Mfuko wa *OPEC*. Mpango kazi wa manunuzi na utekelezaji wa ujenzi huo umeandaliwa na kupitishwa na Mfuko wa *OPEC*. Aidha, tangazo la kukaribisha kampuni za usanifu michoro na usimamizi wa ujenzi limetolewa na kampuni kadhaa zimewasilisha maombi ya kazi na yanaendelea kufanyiwa tathmini.

v) Ujenzi wa vyoo na miundombinu ya maji umekamilika katika Skuli za Mfenesini, Mwanakwerekwe "G" na "H", Chukwani, Kibweni, Kiembesamaki na Pale.

vi) Uandishi wa vitabu vya madarasa ya tano na sita kwa masomo ya Sayansi, Hisabati, *English*, Kiswahili, Historia, Uraia, Jiografia, Michezo, TEHAMA na Mafunzo ya Amali unaendelea.

vii) Ununuzi na usambazaji wa aina mbalimbali za vyakula kwa wanafunzi unaendelea katika skuli 9 za majaribio ambazo ni Mbuyutende, Kijini, Mfurumatonga, Kigunda na Kidagoni kwa Unguja na Makangale, Mkia wa Ng'ombe, Mgogoni na Kinowe kwa Pemba. Mwongozo wa uendeshaji wa mradi wa chakula kwa skuli za msingi umetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wadau wengi wanaosaidia katika utekelezaji wa mradi huo kuuelewa kwa kina.

viii) Vifaa vya kujifunzia masomo ya Hisabati na Sayansi *(Maths and Science Kits)* kwa skuli za msingi vimenunuliwa.

**Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima**

Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano kati ya SMZ na *BADEA* ambao ulitengewa jumla ya Tsh. 4,611,006,260/=, kati ya hizo Tsh.1,200,000,000/= za SMZ na 3,411,006,260/= ni za *BADEA*. Hadi mwezi Mei, 2015, jumla ya Tsh. 844,466,718/= za SMZ ambazo ni sawa na asilimia 70.4 na Tsh. 1,039,947,899/= za *BADEA* sawa na asilimia 14.3 zilipatikana. Utekelezaji wa malengo ni kama hivi ifuatavyo:- Maelezo zaidi ya utekelezaji wa mradi yako katika Ibara ya 16.

i) Ujenzi wa skuli mpya za sekondari za Paje Mtule, Kombeni na Jumbi umekamilika na skuli hizo zimeanza kutumika.

ii) Ujenzi wa skuli mpya za sekondari Kibuteni na Mkanyageni unaendelea.

iii) Mchakato wa kununua vifaa vya maabara na samani kwa skuli mpya za sekondari za Mkanyageni na Kibuteni unaendelea.

iv) Ujenzi wa uzio kuzunguka Skuli ya sekondari ya Lumumba unaendelea.

**Mradi wa Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali**

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka 2014/15, mradi ulitengewa jumla ya Tsh.bilioni 7.5, kati ya hizo shilingi milioni 700,000,000/= za SMZ na Tsh. 6,879,315,870/= kutoka kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*). Hadi kufikia mwezi Mei, 2015, Tsh. 70,553,282/= za SMZ ambazo ni sawa na asilimia 10.1 ya makadirio na Tsh. 299,844,042/= sawa na asilimia 4.4 kutoka kwa *ADB* zilipatikana. Maelezo yanapatikana katika ibara ya 17.

Utekelezaji wa malengo ulikuwa kama hivi ifuatavyo:

i) Zabuni za ujenzi wa vituo vipya viwili vya Mafunzo ya Amali, vituo viwili vya Elimu Mbadala, ukarabati na upanuzi wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar na ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali zilitangazwa, zilifunguliwa na zimefanyiwa tathmini. Ripoti za tathmini zimepelekwa *ADB* kwa kupatiwa uamuzi.
ii) Kazi za uandaaji wa mitaala kwa ajili ya mafunzo ya wakufunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar na wakufunzi wa Mafunzo ya Amali zinaendelea.
iii) Uandishi wa moduli 11 za wanafunzi na miongozo 11 ya walimu kwa ajili ya kufundisha wanafunzi wa vituo vya Elimu Mbadala unaendelea.
iv) Ujenzi wa Kituo cha Elimu Mbadala cha Wingwi Mtemani unaendelea.

**Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi**

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulitengewa jumla ya Tsh. 300,000,000/= za SMZ kwa ujenzi wa dakhalia mpya ya wavulana katika Skuli ya Sekondari ya Ufundi ya Kengeja na ukarabati wa miundombinu ya umeme katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Mradi haukutekelezwa kutokana na ukosefu wa fedha.

**Mradi wa Ujenzi wa Vyuo vya Kiislamu:**

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu unatekelezwa na SMZ kwa kushirikiana na Serikali ya Falme ya Oman wenye lengo la kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Utamaduni wa Kiislamu katika eneo la Chuo cha Kiislamu Mazizini. Gharama za ujenzi zinalipwa na Serikali ya Falme ya Oman moja kwa moja. Kazi za ujenzi zinaendelea vizuri sana. Maelezo zaidi yanapatikana katika ibara ya 20 hadi 25.

**Utafiti:**

Mhe. Mwenyekiti, kazi za utafiti zimeendelezwa katika mwaka 2014/15. Maafisa watatu wa Wizara walishiriki katika mafunzo ya uchambuzi na uandishi wa taarifa za utafiti wa *SACMEQ IV*. Kazi za uchambuzi na uandishi wa ripoti ya utafiti huo kwa nchi zote 15 wanachama wa *SACMEQ* unaendelea. Aidha, Wizara imekamilisha uandishi wa ripoti ya Tathmini ya Elimu kwa Wote kwa kipindi cha miaka 13 (*EFA – End of Decade Assessment 2001–2013*) ambayo imetathmini Malengo ya Milenia na ya Elimu kwa Wote ifikapo mwaka 2015. Nakala 500 za ripoti hiyo zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali wa elimu wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi na Makatibu Wakuu wa Wizara za Zanzibar, watendaji na viongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Vile vile, Wizara imekamilisha uandishi wa ripoti ya utafiti wa tathmini ya hali ya Kisomo cha Watu Wazima ili kubaini maendeleo na changamoto zinazokikabili kisomo hicho. Mbali na tafiti hizi, Wizara pia imefanya utafiti wa kuwatambua walimu wa masomo ya sanaa wenye uwezo wa kusomesha masomo ya sayansi katika ngazi ya sekondari ya awali pindipo kama watapatiwa mafunzo kazini.

**Ukusanyaji na Uchambuzi wa Taarifa za Elimu**

Mhe. Mwenyekiti, wizara imewapatia mafunzo ya takwimu, watakwimu 6 katika ngazi ya cheti. Idadi hiyo itafanya watakwimu waliopatiwa mafunzo kufikia 12. Watakwimu hao watakapomaliza mafunzo yao watapangiwa vituo vya kazi katika Ofisi za Elimu na Mafunzo ya Amali za Wilaya ili kuhakikisha takwimu zinazokusanywa zinakuwa za ubora unaotakiwa. Watakwimu 6 wa awamu ya kwanza wamehitimu mafunzo yao na tayari wamepangiwa kazi katika ofisi za Wilaya za Kusini na Kaskazini "B" kwa Unguja na Wilaya ya Micheweni, Wete na Chake chake kwa Pemba. Aidha, walimu 486, maafisa 20 kutoka Ofisi za Elimu Wilaya na Waratibu wanane wa Vituo vya Walimu walipatiwa mafunzo ya uchambuzi wa taarifa kwa kutumia kompyuta (*EMIS*).

Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imechapisha kitabu cha takwimu (*Statistical Abstract*) kwa miaka mitatu ya 2010 – 2013. Takwimu hizo zimewasilishwa kwa watendaji mbalimbali wa Wizara katika ngazi za kitaifa, kiwilaya na kiskuli. Aidha, Wizara imezijengea

uwezo ofisi zake za Takwimu za Unguja na Pemba kwa kuzipatia vifaa mbalimbali, vikiwemo printa 3, mashine za fotokopi 2 na vespa 2.

**Maendeleo ya Kisera**

Mhe. Mwenyekiti, wizara imeitafsiri kwa Kiswahili Sera ya Elimu ya mwaka 2006 ili kutoa fursa kwa wadau wengi zaidi kuielewa ipasavyo na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Sera hiyo. Jumla ya nakala 500 zimechapishwa na kusambazwa katika skuli za Serikali na za binafsi. Wizara pia, imeiwasilisha Sera hiyo kwa walimu wakuu wa skuli za Serikali na za binafsi kupitia mkutano wa siku moja kwa kila Wilaya.

**Ufuatiliaji na Tathmini**

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, maafisa watano wa Ufuatiliaji na Tathmini wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi ya wiki mbili huko Tanzania Bara. Mafunzo hayo yalilenga kuwaongezea uwezo wao katika masuala ya ufuatiliaji na tathmini. Maafisa hao kwa sasa wanaendelea na kazi za ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya kielimu. Vile vile, Maafisa 21 wa ufuatiliaji na tathmini walipatiwa mafunzo kazini.

Mhe. Mwenyekiti, wizara kupitia Divisheni ya Ufuatiliaji na Tathmini ilifanya kazi kwa karibu na Tume ya Mipango kwa kujengewa uwezo wa utayarishaji wa ripoti ya robo mwaka ya MKUZA II. Aidha, mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa Mpango Mkuu wa Elimu ulitayarishwa na baadhi ya taarifa zimeanza kukusanywa kwa kutumia viashiria vya Mpango Mkuu wa Elimu na viashiria vya Sera ya Elimu ili kutathmini utekelezaji wake kwa lengo la kuzitumia taarifa hizo katika kuandaa Mpango Kazi Mkuu wa Elimu wa miaka mitano 2016 – 2020.

**IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI**

Mhe. Mwenyekiti, idara hii inahusika na masuala yote ya kiutumishi na uendeshaji, kusimamia sheria na kanuni za kazi pamoja na maslahi ya wafanyakazi. Idara pia inahusika na shughuli za kuratibu safari za wafanyakazi wote wa ndani na nje ya nchi, utunzaji wa kumbukumbu za idara na inaratibu mafunzo mbali mbali ya wafanyakazi kulingana na mahitaji ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, jumla ya wafanyakazi 202, walimu 199 (108 Unguja na 91 Pemba) na watumishi wengine 3 waliajiriwa. Kati yao walimu 73 wenye shahada ya kwanza ya Sayansi, 33 wa Shahada ya Sanaa na 1 Cheti cha daraja la 3A na 1 Stashahada ya Ufundi Umeme wameajiriwa kwa skuli za Unguja na kwa Pemba. Walimu wenye Shahada ya sayansi 25, 36 wenye shahada ya sanaa, 2 wa Statashahada ya Sayansi na walimu 30 wa Cheti cha daraja la 3A,

waliajiriwa. Wizara pia iliajiri mhudumu 1 na mlinzi 1 kwa Unguja na fundi bomba 1 kwa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wafanyakazi 1,372 (778 Unguja na 594 Pemba) wenye vyeti na uzoefu wa kazi wa zaidi ya miaka 30 walifanyiwa marekebisho ya mishahara yao, ambapo jumla ya Tsh. 513,561,000/= zilitumika. Pia, jumla ya Tsh. 156,700,000/= zilitumika kuwalipa posho la likizo wafanyakazi 1,567 (1,025 Unguja na 542 Pemba) waliajiriwa. Maelezo zaidi yanapatikana katika ibara ya 29 hadi 32.

Mhe. Mwenyekiti, katika jitihada za kuwaendeleza watumishi wa Wizara yangu, jumla ya wafanyakazi 937 (753 Unguja na 184 Pemba) walipatiwa fursa ya kujiunga na masomo katika vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi katika ngazi tofauti baada ya kukamilisha masharti ya kiutumishi na ya vyuo. Vile vile, wafanyakazi 30 wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi walipatiwa mafunzo kazini, 26 walipatiwa mafunzo maalumu mafupi ya siku 10 ya kuwajengea uwezo katika Chuo cha Utumishi wa Umma cha Tanzania Bara na wafanyakazi 4 wamejiunga na mafunzo ya Stashahada ya Uwekaji wa Kumbukumbu katika Chuo wa Utawala wa Umma cha Zanzibar (*IPA*).

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, jumla ya wafanyakazi 138 walistaafu kwa mujibu wa sheria, wafanyakazi 4 waliacha kazi kwa hiari, wafanyakazi 4 walipewa uhamisho wa kuendelea na kazi katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali, wafanyakazi 27 walichukua likizo bila ya malipo na 10 wamefariki dunia. Mola awalaze mahali pema peponi, Amin.

Hadi kufikia mwezi Mei, 2015 Wizara ilikuwa na jumla ya wafanyakazi 13,852 (8,670 ni wanawake, 5,182 wanaume), wafanyakazi 10,082 wa Unguja (6,839 wanawake na 3,243 wanaume) na 3,770 kwa Pemba (wanawake 1,831 na wanaume ni 1,939). Kati ya wafanyakazi hao, wafanya 12,916 wapo katika kada ya ualimu na 935 wasiokuwa katika kada ya ualimu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuendeleza juhudi za kuwasaidia wafanyakazi wetu katika kujikwamua na matatizo ya kimaisha, Wizara imewadhamini wafanyakazi 662 (462 Unguja na 200 Pemba) kupata mikopo ya fedha taslim, vifaa vya ujenzi, vipando na vifaa vya matumizi ya nyumbani. Thamani ya mikopo yote ni Tsh. 2,232,989,429/=.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuushukuru uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar, Benki ya Posta Tanzania, *CRDB*, Benki ya *Barclays* na *SACCOS* zote kwa kuwapatia mikopo watumishi wa Wizara yangu. Nawaomba waendeleze ushirikiano huo.

## IDARA YA ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi ina jukumu ya kusimamia utoaji wa elimu bora kwa ngazi ya maandalizi na msingi pamoja na uratibu wa elimu ya vyuo vya Kur-ani na madrasa hapa nchini. Aidha, idara inasimamia skuli binafsi za maandalizi na msingi ili kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa na skuli hizo inafuata mtaala ulioidhinishwa na Wizara ya Elimu.

### Elimu ya Madrasa na Vyuo vya Kur-an

Mhe. Mwenyekiti, idara inashughulikia jumla ya Vyuo vya Kur-ani 2,296 na skuli za maandalizi za madarasa za jamii 85 Unguja na Pemba. Skuli hizo zinasimamiwa na kuhudumiwa kupitia Jumuiya ya "*Madrasa Early Childhood Programme''* ambazo ufundishaji wake unafuata misingi ya Dini ya Kiislam.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, walimu 700 wa vyuo vya kur-an (400 kwa Unguja na 300 Pemba) walipatiwa mafunzo yanayohusu mbinu shirikishi za kufundishia, malezi ya Kiislamu na utambuzi wa udhalilishaji wa watoto. Aidha, Vyuo vya Kur-ani 200 pamoja na walimu wa vyuo vya Kur-ani wamepewa miongozo ya ufundishaji wa masomo yanayohusu dini ya Kiislam. Idara pia imefanya ziara ya kuvitembelea vyuo 400 vya Unguja na Pemba na kugawa juzuu 2,000.

### Elimu ya Maandalizi

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15, idadi ya vituo vya maandalizi zimefikia 270 kati ya hivyo 239 vya binafsi ambavyo vina jumla ya wanafunzi 22,801 na vituo 31 vya serikali vyenye jumla ya wanafunzi 18,930. Jumla ya wanafunzi wote walioko katika ngazi hii ni 41,731 wakiwemo wanawake 21,345 na wanaume 20,386 ambayo ni sawa na asilimia 30.7. Jadweli namba 13(a) linatoa ufafanuzi zaidi na maelezo zaidi yanapatikana katika ibara ya 37 hadi 40.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Idara iliendelea kuzisaidia skuli za maandalizi zenye mazingira magumu katika upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama vile chaki, madaftari ya mahudhurio, madaftari ya wanafunzi na manila ili kuwapunguzia wazazi mzigo wa kuchangia ununuzi wa vifaa hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Idara iliwajengea uwezo walimu 350 wa msingi wa Unguja na Pemba ili wawe na uwezo wa kufundisha vizuri madarasa ya maandalizi yanayofunguliwa katika skuli zao. Wizara pia imeyaimarisha maeneo ya kuchezea watoto katika skuli 30 za maandalizi za Unguja na Pemba.

Aidha, wizara kwa kushirikiana na *Madrasa Early Childhood Programme* kupitia ufadhili wa Shirika la Kiraia "*Dubai Care*" imewaendeleza walimu 100 kwa kuwapatia mafunzo ya ualimu wa maandalizi ngazi ya cheti ili watambulike rasmi kuwa ni walimu wa kufundisha katika ngazi hii ya elimu. Pia walimu 154 wa msingi wamepatiwa mafunzo kazini ya elimu ya maandalizi yaliyowezesha kufunguliwa madarasa 48 ya maandalizi katika skuli 48 za msingi, 30 kati ya skuli hizo ziko Pemba. Aidha, kupitia programu ya "*Madrasa Early Childhood"* walimu 17 wa msingi wamepatiwa mafunzo ya jinsi ya kuwapokea wanafunzi wanaotoka katika madarasa ya maandalizi kwa wilaya ya Mjini na Magharibi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara katika mwaka 2014/15, iliendelea kutoa elimu ya maandalizi kwa njia ya redio (*ZBC*) kupitia programu za "*Tucheze Tujifunze*" (TUTU). Jumla ya vituo 51 vipya vya TUTU vimeanzishwa katika Wilaya za Kaskazini 'B' Unguja na Wilaya ya Mkoani, Pemba. Vituo hivyo vinasimamiwa na walimu wasaidizi 102, ambao wanawaongoza wanafunzi kulingana na maelekezo yanayotolewa na wakufunzi kupitia *ZBC* redio. Kwa kupitia njia ya redio, watoto 7,871 wameweza kupata elimu ya maandalizi hasa vijijini ambako bado skuli za maandalizi ziko chache. Jadweli namba 13(c) linatoa ufafanuzi zaidi. Juhudi za kuielimisha jamii kuhusu umuhimu na faida za kuwaandikisha watoto katika skuli za maandalizi wanapotimia umri wa miaka minne zinaendelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa kushirikiana na *UNICEF*, iliandaa Mkutano wa Kimataifa wa Elimu bora ya Maandalizi uliofanyika *Zanzibar Beach Resort* na ulilenga kuzungumzia haki za mtoto, mazingira yake na namna ya kujifunza. Washiriki 160 kutoka nchi za Afrika zilizo chini ya Jangwa la Sahara walihudhuria mkutano huo.

**Elimu ya Msingi**

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Mei 2015, Elimu ya Msingi inatolewa katika skuli 370 zikiwemo skuli 273 za serikali na 97 za binafsi. Idadi ya wanafunzi katika ngazi hii imefikia 261,212 sawa na asilimia 98.4 ikilinganishwa na wanafunzi 252,938 sawa na asilimia 102.5 wa mwaka uliopita. Kati yao wanawake ni 131,226 na wanaume 129,986. Jumla ya wanafunzi 36,608 walioandikishwa kuanza darasa la kwanza katika skuli za serikali wamepatiwa nafasi. Miongoni mwa watoto hao 17,742 ni wanawake na 18,866 ni wanaume. Jadweli namba 14 na 15 zinatoa uchambuzi zaidi na maelezo zaidi yanapatikana katika ibara ya 42 hadi 44.

Mhe. Mwenyekiti, walimu 20 walipatiwa mafunzo ya kusimamia klabu za afya katika skuli. Wizara pia, ilishirikiana na Wizara ya Afya kupitia kitengo cha malaria, kuwapatia mafunzo walimu 24, wanafunzi 24 na Maafisa Elimu Mikoa wa

Unguja juu ya mbinu za kujikinga na maradhi ya malaria kwa jamii na kusaidia kuufikia mkakati wa kumaliza malaria nchini.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Wizara kwa kushirikiana na Shirika linaloshughulikia maendeleo ya watoto "*Partnership for Child Development* (*PCD*)" la Uingereza, imeanzisha mpango wa majaribio wa kutoa chakula katika skuli 9 za msingi za Unguja na Pemba. Skuli hizo ni Mfurumatonga, Kijini, Kidagoni, Kigunda na Mbuyutende katika wilaya ya Kaskazini "A", Unguja na Makangale, Mgogoni, Mkia ng'ombe na Kinowe katika Wilaya ya Micheweni, Pemba. Malengo ya mpango huu ni kupunguza utoro kwa wanafunzi, kuongeza utulivu na ufahamu wa masomo kwa wanafunzi pamoja na kuongeza kipato cha wakulima wadogo wadogo, kwani vyakula vinavyoliwa na wanafunzi hawa vinanunuliwa kutoka kwa wakulima wadogo wadogo katika maeneo husika.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Idara ilifanya mikutano miwili ya kuhamasisha jamii juu ya kupambana na utoro wa wanafunzi katika wilaya ya Mjini na Magharibi. Jumla ya wanajamii 100 walifikiwa katika uhamasishaji huo wakiwemo wajumbe wa kamati za skuli, masheha na wazazi wa wanafunzi. Uhamasishaji huu unatarajiwa kusaidia kuongeza uwelewa wa jamii juu ya umuhimu wa watoto kubakia darasani badala ya kuachwa kuzurura au kujiwekeza katika shughuli za kiuchumi (ajira za watoto).

## IDARA YA ELIMU YA SEKONDARI

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa kazi za ufundishaji kwa ujumla, kupanga walimu katika skuli zote za sekondari za serikali, kuwapangia skuli wanafunzi waliofaulu kuendelea na masomo ya sekondari katika ngazi mbali mbali, kusaidia usimamizi wa shughuli za uzalishaji mali na uwekaji wa kumbukumbu za mapato na matumizi ya skuli, kufuatilia utendaji wa serikali za wanafunzi na huduma za dakhalia.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Elimu ya Sekondari ilikuwa inatolewa katika skuli 263 kati ya hizo skuli 208 ni za serikali na 55 za binafsi. Skuli hizo zilikuwa na jumla ya wanafunzi 86,969 kuanzia Kidato cha Kwanza hadi Kidato cha Sita. Kati yao, wanaume ni 40,176 na wanawake ni 46,793. Wanafunzi waliokuwepo katika ngazi ya elimu ya lazima kidato cha 1 na cha 2 ni 55,523 (wanawake 29,326 na wanaume 26,197) ambao ni sawa na asilimia 76.3 ya watoto wenye umri wa miaka 14 – 15 wanaotarajiwa kuwepo skuli. Kwa upande wa kidato cha 3 na cha 4 wanafunzi 21,658 (12,295 wanawake na 9363 wanaume) walisajiliwa skuli za serikali na 2,648 (1402 wanawake na 1246 wanaume) wa skuli za binafsi. Pia wanafunzi 2,640 wa kidato cha 5 na 6, kati yao 1,460 wanawake (2,375 wa serikali na 265 wa binafsi) walipata fursa ya kujisomea.

Jadweli namba 16 - 22 yanatoa uchambuzi zaidi na maelezo zaidi yanapatikana katika ibara ya 47 hadi ya 50.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Idara ilinunua kompyuta 50, mashine za fotokopi 3 na projekta 2 kwa ajili ya skuli za sekondari za michepuo ya Kompyuta na Biashara. Idara pia, imenunua vifaa vya maabara za sayansi kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi kufanya mazoezi ya vitendo wakati wa kujifunza. Vifaa hivyo vilisambazwa katika skuli 145 zenye kidato cha 4 (Unguja 95 na 50 Pemba) na skuli 6 za sekondari ya juu (4 Unguja na 2 Pemba). Idara pia ilipokea msaada wa kompyuta 50 kutoka katika Kampuni ya *ZTE* ya China na mafeni 30 kutoka kwa Mbunge wa Jimbo la Kiembesamaki kwa skuli ya sekondari ya Kiembesamaki.

Aidha, idara imeongeza fursa kwa wanafunzi ya kujifunza fani ya michezo, upishi na ushoni, uchoraji na lugha ya Kifaransa. Masomo hayo yanatarajiwa kuzalisha rasilimali watu wenye utaalamu wa msingi katika fani husika wanaohitajika nchini. Hadi mwezi Mei, 2015, somo la michezo limeanza kufundishwa katika skuli 10, lugha ya Kifaransa kwa wanafunzi wasio wa michepuo inafundishwa katika skuli 5 na uchoraji katika skuli 3, wakati ushoni na upishi katika skuli moja.

**Serikali za Wanafunzi**

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Idara ilitoa mafunzo juu ya wajibu na maadili ya wanafunzi, mapambano dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia, kujiepusha na vitendo vya uasharati, athari za matumizi ya madawa ya kulevya na mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI. Aidha, Serikali za Wanafunzi kwa upande wake zinaendelea kutekeleza majukumu yao ya kuwasimamia wanafunzi katika upatikanaji wa elimu bora. Shughuli wanazozitekeleza ni pamoja na kusimamia usafi wa skuli, nidhamu na kuhakikisha walimu wanaingia madarasa kwa mujibu wa vipindi vyao.

**Huduma za wanafunzi**

Mhe. Mwenyekiti, hadi mwezi Mei 2015, idadi ya wanafunzi waliopo dakhalia imefikia 1921, kati yao wanaume 1,048 na wanawake 873. Katika kuimarisha huduma za dakhalia zetu, Idara inatayarisha mwongozo wa kuchukua wanafunzi watakaoishi dakhalia.

**Kazi za Ujasiriamali**

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, shughuli za ujasiriamali katika skuli zetu ziliendelea kama kawaida na fedha zinazopatikana zinatumika kutatua matatizo ya kitaaluma na kijamii yanayojitokeza skuli. Jumla ya walimu

wajasiriamali 145 walipatiwa mafunzo ya utunzaji bora wa kumbukumbu za mapato na matumizi.

## IDARA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO KATIKA ELIMU

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ina jukumu la kuandaa na kusimamia Sera ya TEHAMA katika Elimu, kusimamia matumizi sahihi ya TEHAMA katika kujifunza na kufundishia katika ngazi mbal mbali za elimu, kuimarisha huduma ya mawasiliano na usalama wa taarifa, kuratibu na kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu na watumishi wengine wa Wizara ya Elimu na kuandaa programu mbali mbali za kompyuta ambazo zitaongeza ufanisi wa shughuli za wizara.

### Sera ya TEHAMA katika Elimu

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2014/15 Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika elimu ilikamilisha rasimu ya mwisho ya Sera ya TEHAMA katika elimu na sasa ipo tayari kupelekwa Serikali Kuu kwa kuthibitishwa. Matayarisho ya awali ya kuandika Mpango Mkakati wa Sera ya TEHAMA katika Elimu yameanza.

### Kuimarisha Matumizi Sahihi ya TEHAMA katika Kujifunza na Kufundishia

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya watendaji 54 wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali walipatiwa mafunzo mafupi ya TEHAMA ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, 32 walipatiwa mafunzo katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, 17 walipatiwa mafunzo ya kitaalamu juu ya uendeshaji na usimamizi wa mtandao wa kompyuta yaliyoendeshwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na watendaji 5 wamepatiwa mafunzo mafupi nje ya nchi yaliyohusu matumizi ya teknolojia katika kujifunza na kufundishia. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo na kuimarisha ufanisi wa kazi za kila siku. Pia mafunzo hayo yalilenga kutatua baadhi ya changamoto zinazowakabili wafanyakazi wakati wa matumizi ya TEHAMA. Maelezo zaidi yanapatikana katika ibara ya 54 hadi 56.

### Utekelezaji wa Mradi wa *(TZ -21*)

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, mradi huu uliendesha mafunzo mbalimbali yaliyohusu mbinu bora za kufundishia na matumizi na utunzaji wa vifaa vya TEHAMA vilivyotolewa na mradi huo. Hivyo, jumla ya watendaji 8, kati ya hao 5 ni kutoka Unguja na 3 Pemba walipatiwa mafunzo mafupi ya ufundi wa vifaa vya TEHAMA vilivyotumika katika mradi huu. Walimu 974 na Maafisa 21 walishiriki mafunzo ya kuhimiza kusoma na mbinu bora za kufundisha darasa la kwanza na la pili. Aidha, *TZ-21* kwa mashirikiano na "*Children Book*

*Publishers*”waliandika aina 5 za vitabu vyenye maudhui tofauti na kuchapisha nakala 43,700 na kuzigawa kwa skuli 248 za msingi ambazo zimo katika mradi. Pia, mgao huo ulilenga vituo vyote vya walimu, Ofisi za Elimu Mkoa na Wilaya, Ofisi ya Taasisi ya Elimu Zanzibar, Ofisi za *TZ-21* na Children Book Publishers.

**Kuimarisha Njia za Mawasiliano na Usalama wa Taarifa kupitia TEHAMA**

Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa mashirikiano na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Ofisi ya Serikali ya Mtandao (*e-Government Office*), Zantel na *ZTE* inaendelea na jitihada za kuziunganisha taasisi zake na mkonga wa Taifa. Vituo vyote vya Walimu vimekaguliwa kwa nia ya kuviunganisha na mkonga wa Taifa ili hatimae navyo viunganishe skuli wanazozihudumia. Sambamba na hilo, matumizi ya tovuti ndani ya Wizara yameimarishwa. Tovuti inatumiwa kutoa taarifa za elimu kwa wananchi na wadau wa elimu. Taarifa hizi ni pamoja na zile zinahusu utendaji wa Wizara, fursa za masomo nchini na nchi za nje, taarifa za matokeo ya mitihani ya darasa la saba, kidato cha Pili, cha Nne na kidato cha Sita.

**Ufuatiliaji na Tathmini**

Mhe. Mwenyekiti, idara katika kipindi cha 2014/15, ilifuatilia skuli 203 (78 za Unguja na 125 za Pemba) kuangalia utunzaji na matumizi ya vifaa vya TEHAMA katika kujifunza na kufundishia. Mafanikio makubwa yaliyopo katika sekta hii ni mwamko wa walimu, wanafunzi na jamii kwa ujumla juu ya kupenda kutumia teknolojia hii. Hata hivyo, matumaini haya mazuri yamekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo, uhaba na uchakavu wa vifaa.

**IDARA YA ELIMU MBADALA NA WATU WAZIMA**

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ina jukumu la kuondoa tatizo la kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wananchi wote, kuwapatia elimu mbadala vijana walioacha masomo njiani na wale ambao hawakubahatika kabisa kupata masomo ya msingi.

**Kisomo**

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, jumla ya madarasa mapya 9 ya kisomo yamefunguliwa Unguja na Pemba. Idadi ya madarasa ya kisomo ni 440 yenye wanakisomo 7,331 wakiwemo wanawake 6,257 na wanaume 1,074. Jumla ya wanakisomo 6,225 wamefanyiwa upimaji katika hatua zote nne na wanakisomo 448 wa hatua ya nne wamekombolewa. Aidha, katika kuyaendeleza madarasa yaliyopo vifaa mbali mbali vya kujifunzia na kufundishia vilitolewa yakiwemo mabuku, penseli, mbao, chaki, mistari, miwani kwa wanakisomo wenye matatizo ya macho Unguja na Pemba.

**Elimu Mbadala**

Mhe. Mwenyekiti, Elimu Mbadala inalenga kuwapatia elimu vijana wenye umri kati ya miaka 10 hadi 15 walio nje ya skuli, wakiwemo walioacha masomo njiani kutokana na sababu mbali mbali. Katika mwaka 2014/15, jumla ya wanafunzi 734 (288 Pemba na 446 Unguja), wanahudhuria masomo ya elimu mbadala katika madarasa 21 Unguja na 19 Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo, kina jumla ya vijana 403 (wanawake 100 na wanaume 303) ambao wanasoma masomo ya kawaida na mafunzo ya fani mbalimbali zikiwemo ushoni, upishi, umeme, uchongaji, udobi, mafunzo ya kompyuta na utunzaji wa nyumba. Kituo hiki hadi sasa, kimeshatowa wahitimu 3,438 tangu kuanzishwa, (wanawake 2,409 na wanaume 1,029) wa fani mbalimbali ambao wametunukiwa vyeti. Fani zinazofundishwa zina nafasi nzuri katika soko la ajira.

**Vituo vya Kujiendeleza**

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, jumla ya wanafunzi 2,434 (wanawake 1,191 na wanaume 1,243) wamesajiliwa katika Vituo mbalimbali vya kujiendeleza Unguja na Pemba. Wanafunzi 4,658 wamefanya mtihani wa faragha wa kidato cha Nne ambapo wanafunzi 1,891 sawa na asilimia 40.6 ya watahiniwa wote wamefaulu. Kwa mwaka wa masomo 2013/14, jumla ya wanafunzi 745 wa Unguja na Pemba walifanya mtihani wa faragha wa kidato cha sita, kati yao wanawake ni 403 na wanaume ni 342, watahiniwa 217 ambao ni sawa na asilimia 29.1 walifaulu.

Mhe. Mwenyekiti, kituo cha sayansi kimu, kilichopo Forodhani kina jumla ya vijana 127 (106 ni wanawake). Vijana hawa wanafundishwa fani mbalimbali ikiwemo upishi, ushoni, kudarizi, kufuma, kompyuta na uchongaji. Tokea kuanzishwa kwa kituo hiki, wahitimu 2,350 wamehitimu mafunzo yao na wengi wao wameajiriwa na wengine wamejiajiri wenyewe. Aidha, mpango wa majaribio wa *YELP* (Y*outh Empowerment of Life Program)* katika wilaya ya mjini ambao husomesha vijana masomo ya lugha, ujasiri amali, umeme na utunzaji wa nyumba umeonesha mafanikio kwa kutoa wahitimu 165 (wanawake 84 na wanaume 81) waliotunukiwa vyeti.

**Programu za Wanawake**

Mhe. Mwenyekiti, idara hii pia ina jukumu la kuwahamasisha wananchi na hasa wanakisomo waliofikia hatua ya nne kujiunga na vikundi vya programu za wanawake ili kujikwamua na tatizo la umasikini kwa kujiongezea kipato. Idara ina jumla ya vikundi 103 vyenye wanachama 2,097 (vikundi 73 vipo Unguja na 30

Pemba). Vikundi hivyo vimepatiwa vifaa mbalimbali vikiwemo vyerehani 8, majembe, keni za kumwagilia maji na viatu.

**Vyombo vya Habari**

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Idara ilirusha hewani vipindi 15 vya redio na kimoja cha TV. Idara pia, iliandaa makala moja iliyochapishwa katika gazeti la Zanzibar Leo.

**IDARA YA MAFUNZO YA UALIMU**

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ina jukumu la kusimamia mafunzo ya ualimu vyuoni na mafunzo ya ualimu kazini. Mafunzo ya ualimu hutolewa katika vyuo vitatu navyo ni Chuo cha Kiislamu Mazizini Unguja, Chuo cha Kiislamu Kiuyu Pemba na Chuo cha Benjamin William Mkapa huko Mchangamdogo. Vyuo hivi vinatoa mafunzo ya ualimu ya Stashahada ya Sanaa, Stashahada ya Sayansi kwa sekondari, Stashahada ya Ualimu Msingi, Stashahada ya somo la Dini na Kiarabu na Cheti cha Ualimu wa Elimu Mjumuisho. Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, vyuo hivi vilikuwa na jumla ya wanafunzi 750 (wanaume 166 na wanawake 584). Jadweli namba 30 (a)-(c) zinatoa ufafanuzi zaidi.

**Mafunzo ya Ualimu Kazini**

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa mafunzo ya ualimu kazini yanawafikia walimu wengi, wizara inatumia vituo vya walimu vya kila wilaya kuwaendeleza walimu kitaaluma ili wamudu vyema kazi yao ya ufundishaji. Kila kituo husimamia skuli ambazo zimo katika klasta yake. Hivi sasa vipo vituo vya walimu kumi na tatu, viwili kati ya hivyo ni vituo vya walimu wa maandalizi na kimoja ni Kituo cha Taifa cha Walimu (*NTRC*). Katika mwaka 2014/2015, idara imeanzisha kituo kipya cha walimu huko Mwanda ambacho kinahudumia baadhi ya skuli za Wilaya ya Kaskazini "B". Vituo hivi sasa vinatoa mafunzo kwa walimu katika masomo mbalimbali.

Mhe. Mwenyekiti, katika juhudi za kuimarisha ufundishaji wa masomo ya Sayansi, Idara inashirikiana na jumuiya ya "*Strengthening of Mathematics and Science Education in Africa* (*SMASE Africa*)" kutoa mafunzo ya mbinu za ufundishaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa walimu wa Zanzibar. Walimu wanne walishiriki katika mafunzo ya wiki tatu nchini Kenya yanayohusiana na mbinu za ufundishaji wa Sayansi na Hisabati. Walimu hawa watakuwa wakufunzi wa kuendesha mafunzo kwa walimu wa Sayansi na Hisabati waliomo katika skuli zetu.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya kutambua mada ngumu katika somo la Hisabati, Sayansi na Kiingereza kwa madarasa ya juu ya msingi ilitekelezwa na watafiti kutoka *SUZA*. Ripoti ya kazi hiyo iliwasilishwa na kujadiliwa kwa wadau mbalimbali wa elimu kabla ya kuwasilishwa rasmi kwa viongozi wa Wizara. Idara ya Mafunzo ya Ualimu imeitumia ripoti hiyo kwa kuandaa moduli pamoja na kutoa mafunzo kwa wakufunzi 23 Unguja na 18 Pemba. Kwa mwaka 2014/15, walimu 300 walipatiwa mafunzo katika vituo vya walimu vitano vya Kitogani, Mkwajuni na Bububu kwa Unguja na kwa Pemba ni Miti-Ulaya na Mizingani ambapo kila kituo kilitoa walimu 60; walimu 20 kwa kila somo.

Mhe. Mwenyekiti, idara kwa kushirikiana na kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za maisha imetoa mafunzo yanayohusiana na elimu mjumuisho, stadi za maisha na mambo mtambuka. Jumla ya walimu 240 (140 Unguja, 100 Pemba) wamepatiwa mafunzo hayo. Idara pia, inaratibu na kusimamia mafunzo ya miaka miwili yanayoendeshwa kwa kutumia mbinu ya TEHAMA katika vituo vyote 12 vya walimu Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yanalenga kuwatayarisha walimu wa kufundisha madarasa ya maandalizi. Jumla ya walimu 352 (202 Unguja na 150 Pemba) wanashiriki mafunzo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Idara imeshirikiana na mashirika mbalimbali katika kuendesha mafunzo kazini kwa walimu wa ngazi tofauti. Walimu 500 wa sekondari (Unguja 300 na Pemba 200) wamepatiwa mafunzo ya kuinua uwezo wao wa kufundisha masomo ya Hisabati na Sayansi. Walimu 300 (wanaume 145 na wanawake 155) wa Sayansi darasa la 5 na 6 walipatiwa mafunzo ya kukuza lugha ya kiingereza na mawasiliano katika vituo 10 Unguja na Pemba. Idara kwa kushirikiana na Ubalozi wa Marekani inaendesha mafunzo ya lugha ya Kiingereza na mbinu za kufundisha kwa njia ya mtandao (*online study*) na walimu 350 kutoka Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya mbinu za kufundisha madarasa ya maandalizi.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya walimu 565 kati yao, 351 wa Unguja (wanawake 331) na walimu 214 wa Pemba (wanawake 175) wa mkupuo wa nne wamekamilisha mafunzo ya Cheti cha ualimu Daraja la IIIB kwa njia ya elimu masafa katika vituo tisa vya walimu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, idara inaendelea na juhudi zake za kuwaelimisha wafanyakazi wake. Wakufunzi wanane wa vyuo vya ualimu wamekwenda masomoni ambapo wawili wamejiunga na shahada za uzamivu, 5 wanachukua shahada za uzamili na 1 shahada ya kwanza ya Elimu Mjumuisho. Wafanyakazi 2 wanaendelea na mafunzo ya uzamili kupitia Chuo Kikuu Huria na wafanyakazi 10 wamepata mafunzo mafupi ya kuandika miradi na utafiti.

**IDARA YA MICHEZO NA UTAMADUNI**

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ni mpya na imeanzishwa kwa lengo la kutekeleza Sera ya Taifa ya Michezo katika skuli na kuibua, kukuza, kuimarisha na kuendeleza vipaji vya wanafunzi ili kupata wanamichezo bora katika taifa letu. Idara imechukua nafasi ya Kitengo cha Michezo na Utamaduni ambacho kilikuwa na majukumu hayo.

Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi walishiriki katika mashindano ya skuli za Sekondari Afrika Mashariki (*FEASSSA*) yaliyofanyika Dar es salaam**.** Timu zilizoshiriki ni za mpira wa miguu, wanaume, mpira wa mikono na wavu wanaume zilizoshika nafasi ya tatu katika makundi yaliyozijumuisha timu za Kenya, Uganda, Sudan ya Kusini na Rwanda. Mchezo wa riadha, timu yetu ilishika nafasi ya nne kiujumla.

Pia, idara iliandaa mashindano ya tatu ya riadha ya mbio za nyika *"Elimu Cross Country"* kwa wanafunzi wa skuli za msingi na sekondari, yaliyofanyika mwezi Machi 2015. Jumla ya wakimbiaji 370 wa skuli za msingi na 296 wa sekondari walishiriki, ambapo wanafunzi watano walitoka skuli ya msingi *Filbert Bay* ya Kimara na watano ni kutoka skuli ya sekondari *Filbert Bay* ya Kibaha. Mashindano hayo yameibua hamasa na ushindani mkubwa miongoni mwa wanafunzi kushiriki na hivyo kuongezeka kwa idadi ya washiriki kila mwaka. Mashindano haya mbali ya kuibua hamasa ya kupenda michezo pia yanasaidia kukuza ushirikiano kwa wanafunzi. Idara itaiendeleza michezo hii kila mwaka kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, idara ilishirikiana na Taasisi ya Elimu Zanzibar kutoa mafunzo kwa walimu wanaofundisha somo la michezo katika skuli za msingi juu ya matumizi ya Kadi za Michezo (*TOPs Card)* zilizoandaliwa kwa ajili ya kufundishia. Jumla ya walimu 574 (352 Unguja na 222 Pemba) walifaidika na mafunzo hayo. Mbali na mafunzo kwa walimu, Idara ilifanya kazi ya kuwahamasisha wanafunzi kupenda michezo na kuunda klabu za michezo katika skuli zao. Uongozi wa Idara pia, ulifanya mazungumzo na walimu wakuu na walimu wengine wa skuli za Unguja katika Wilaya ya Kusini, Kati, Mjini na Kaskazini "A" na "B" juu ya umuhimu wa kuwepo harakati za michezo katika skuli zao ikiwa ni pamoja na kufuatilia ili kuona utekelezaji wa mafunzo yanayotolewa.

Mhe. Mwenyekiti, tamasha la miaka 50 ya Elimu Bila ya Malipo liliadhimishwa kwa shughuli mbalimbali zikiwemo za michezo na utamaduni kuanzia ngazi ya Kanda, Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Wanafunzi walishiriki kikamilifu katika shughuli za michezo na utamaduni na kuonesha vipaji vyao katika tasnia hizo. Ushiriki wao umesaidia kufanyika kwa tathmini ya jumla ya shughuli za michezo na mafunzo yanayotolewa.

Mhe. Mwenyekiti, timu zetu za mpira wa miguu kwa wanaume na wanawake, mpira wa kikapu, mpira wa wavu, netiboli, mpira wa mikono, riadha, mpira wa meza, ngoma, kwaya, maigizo na bao zinaendelea na maandalizi ya mashindano ya UMISSETA yatakayofanyika huko Butimba Mwanza kuanzia tarehe 09/06/2015.

## OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ilitekeleza majukumu yake kwa kuzifanyia ukaguzi skuli 376 (286 za serikali na 90 za binafsi) na kuzipitia ripoti za ukaguzi unaofanywa na walimu wakuu. Miongoni mwa yaliyojitokeza katika kaguzi hizo ni baadhi ya walimu wakuu kwa kushirikiana na walimu wao wanasimamia vyema upatikanaji na utoaji wa elimu bora katika skuli zao kwa kiwango cha kuridhisha. Hata hivyo, ilijitokeza kwamba baadhi ya walimu wakuu wanakabiliwa na changamoto nyingi za kiutendaji, zikiwemo uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati. Hali iliyopelekea walimu wa sanaa kusomesha masomo ya sayansi. Skuli nyingi zinakabiliwa na tatizo la kutokuwa na hati miliki na kupelekea uvamizi wa maeneo ya skuli husika.

Mhe. Mwenyekiti, **o**fisi kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, wanasheria pamoja na wadau wengine imeendelea na mchakato wa kuandika sheria ya kuanzishwa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu kwa kuandika waraka rasmi (*concept paper*) kwa ajili ya kuwasilishwa katika kikao cha makatibu wakuu na baadae kufikishwa katika ngazi zinazofuata kisheria. Mswada huu unatarajiwa kuwa sheria kamili katika mwaka wa 2015/16. Kumalizika kwa sheria hii, kutaiwezesha Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu kuwa na mamlaka ya kuanzisha ofisi za ukaguzi za wilaya na kufanya ukaguzi kwa kanda utaopelekea skuli nyingi kukaguliwa kwa wakati na kuongeza ufanisi katika utendaji na uwajibikaji.

Mhe. Mwenyekiti, matayarisho kwa ajili ya ukaguzi wa kanda yameanza kwa kununua vifaa vya kufanyia kazi za ofisi za kanda/wilaya zikiwemo komputa 10, printa 10, scanner 10, meza 10 na viti 20.

## TAASISI YA ELIMU ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu Zanzibar ina majukumu ya kubuni na kuandaa mitaala na mihutasari ya elimu ya maandalizi, msingi, sekondari, ualimu na elimu ya kujiendeleza nje ya mfumo rasmi. Katika mwaka 2014/2015, Taasisi ya Elimu Zanzibar ilikamilisha uandishi wa viwango vya kujifunzia (*achievement standards*) kwa elimu ya msingi na sekondari ya awali (kidato cha 1 na cha 2). Taasisi pia, ilitoa mafunzo ya namna ya kutumia viwango vya kujifunza kupima maendeleo ya wanafunzi kwa washauri wa masomo 34 (20 kutoka Unguja na 14 Pemba). Taasisi iliandaa mafunzo ya namna ya kutumia viwango hivyo kupima maendeleo ya mwanafunzi kwa walimu wa msingi 3,532 (1,071 kutoka Pemba na 2,461 Unguja).

Aidha, ilitoa mafunzo ya mtaala mpya kwa washauri wa masomo 29 (15 Unguja na 14 Pemba).

Mhe. Mwenyekiti, Pia Taasisi ya Elimu iliandaa mafunzo ya matumizi ya mtaala mpya kwa walimu 450 (290 Unguja na 160 Pemba) wanaofundisha madarasa ya 5 na 6. Vile vile, Taasisi ilitayarisha vigezo kwa ajili ya uandishi wa vitabu vya maandalizi, msingi kwa darasa la tano na sita na ilitayarisha vigezo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia Sayansi na Hisabati (*Science and Mathematics Kits*). Aidha, taasisi ilifanya upembuzi yakinifu wa matayarisho ya mtaala wa walimu wa maandalizi.

**MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI**

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali inaendelea kutoa, kusimamia na kuratibu shughuli zote za elimu ya mafunzo ya amali hapa Zanzibar. Katika mwaka 2014/15, jumla ya wanafunzi 468 (132 wanawake na 336 wanaume) wanahudhuria mafunzo ya kazi za amali katika vituo vitatu vya serikali vya Mkokotoni, Mwanakwerekwe na Vitongoji. Vijana hawa wanajifunza fani mbalimbali za ufundi zikiwemo useremala, ushoni, uhunzi, upishi, uchoraji na uandishi wa alama, uashi, ufundi bomba, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, huduma za chakula na vinywaji, elektroniki, ufundi magari, umeme na ufundi mafriji na viyoyozi. Jadweli Namba 40(a) linatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2015, Mamlaka imeendelea na ukaguzi wa vituo vya mafunzo ya amali vya binafsi na vya serikali. Jumla ya vituo vya amali 20 vimefanyiwa ukaguzi wa kawaida kuangalia kwa makini mafunzo yanayotolewa yanakidhi mahitaji na vituo 10 vimefanyiwa ukaguzi kwa ajili ya usajili baada ya kukamilisha kujaza fomu za maombi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2015, Mamlaka imeajiri wafanyakazi 8 (wanawake 3 na wanaume 5) kati yao, walimu 5 na maafisa 3. Pia katika kuviimarisha vituo Mamlaka imeajiri Afisa uzalishaji mali ambaye atasimamia uzalishaji na ukusanyaji wa mapato katika vituo vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, Tarehe 29 Disemba, 2014 Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ilifanya mahafali ya kwanza ambapo jumla ya wahitimu 239 (wanawake 94 na wanaume 145) walitunukiwa vyeti baada ya kukamilisha mafunzo ya miaka mitatu katika vituo vya Mkokotoni, Mwanakwerekwe na Vitongoji. Mamlaka pia inaratibu shughuli mbalimbali za Mitihani ya Taifa ya ufundi stadi "*CBA*" na "*Competency Based Education and Training*" (*CBET*) ya Tanzania Bara, jumla ya vijana 754 walifanya mitihani hio, kati yao 378 walifaulu ikiwa ni sawa na asilimia 50.13. Katika kujenga uwezo wa wafanyakazi, wafanyakazi 4 wanahudhuria

masomo kutoka ngazi ya cheti na kuendelea na Diploma. Jadweli namba 41(a) - 41(c) yanatoa ufafanuzi zaidi.

## TAASISI ZA ELIMU YA JUU

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, zilikuwepo jumla ya taasisi nne za elimu ya juu. Kati ya hizo, mbili zinamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mbili ni taasisi binafsi.

## TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ni Taasisi inayotoa huduma za kielimu za uhandisi katika ngazi ya Stashahada (*NTA level 4 – NTA level 6*) na pia mafunzo ya kujiendeleza katika fani mbalimbali za ufundi. Taasisi inajukumu la kuendeleza na kukuza elimu ya uhandisi, sayansi na teknolojia ndani ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii ina jumla ya wanafunzi 1,444 (wanawake 303 na wanaume 1,141), kati ya hao wanafunzi 342 wanajifunza Stashahada ya ufundi (wanaume 252 na wanawake 90), 69 Stashahada ya TEHAMA (wanaume 44 na wanawake 25). Vile vile, wapo wanafunzi 765 wanaojifunza mafunzo ya amali (733 wanaume na 32 wanawake). Aidha, wapo wanafunzi 131 (wanaume 94 na wanawake 37) wanaofanya matayarisho ya kujiunga na Stashahada ya Ufundi kwa mwaka 2015/16. Aidha, taasisi inawapatia mafunzo walimu wa msingi 137 ya kuwaongezea uwezo wa kufundisha masomo ya Sayansi na Hisabati kwa elimu ya msingi (119 wanawake na 18 wanaume).

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, taasisi ilikamilisha baadhi ya malengo iliyojiwekea ikiwemo kuanzisha mafunzo kwa wajasiri amali kwa wahitimu kutoka vyuo na sehemu tofauti nchini. Mafunzo hayo yalitolewa kwa mashirikiano na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Mafunzo hayo yanalenga kuwalea (*Business incubator*) na hatimae wahitimu waweze kujiajiri, kuajiri wengine au kuajiriwa. Aidha, taasisi iliimarisha miundombinu ya nishati ya umeme, ilikamilisha ukarabati wa miundombinu ya umeme kwa dakhalia zote mbili. Pia, Taasisi iliwapatia mafunzo ya Shahada ya Pili wakufunzi 7 na wasio wakufunzi 5, Shahada ya kwanza 3, ya pili mmoja na Cheti mmoja.

## CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kimefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kutekeleza shughuli zake kuu ambazo ni kufundisha, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaaluma. Chuo kimetimiza miaka 13 tangu kuanzishwa kwake na kina jumla ya wanafunzi 2,538, programu za masomo 29 kati ya hizo 1

ni ya Shahada ya Uzamivu, 4 Shahada ya Uzamili, 11 za Shahada ya kwanza, 11 za stashahada na 2 za cheti.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa masomo 2014/2015 Chuo kilianzisha programu mpya sita (6), nazo ni za Stashahada ya Elimu Mjumuisho na mahitaji maalum, Stashahada ya Elimu ya Michezo, Shahada ya kwanza ya Sanaa katika Huduma na Utalii, Shahada ya kwanza katika fani ya Sayansi ya Teknolojia ya Habari na Ualimu, Shahada ya Uzamili wa Usimamizi wa Biashara na Shahada ya Uzamili ya Kiswahili. Chuo kimeanza awamu ya pili ya kozi ya uzamivu (*PhD*) ya Kiswahili ambapo wanafunzi 10 wamejiunga na kozi hiyo. Pia, wanafunzi wageni 124 (wanaume 53 na wanawake 71) wamejiunga na Chuo kwa ajili ya kujifunza lugha ya Kiswahili kwa wageni. Jadweli namba 26 (a) na 26(c) yanatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, chuo kilifanya mahafali yake ya 10 tarehe 20 Disemba, 2014. Katika mahafali hayo, Mkuu wa Chuo ambaye ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein aliwatunuku shahada, stashahada na vyeti wahitimu 741, wakiwemo wanaume 266 na wanawake 475 waliohitimu katika programu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo kimeajiri wafanyakazi 12 kati yao 5 wa kada ya taaluma na 7 wafanyakazi wa kada ya uendeshaji. Aidha, Chuo kimeendelea kuwalipia ada za masomo wafanyakazi wake 54 ambao wapo masomoni kwenye ngazi za shahada ya Uzamivu (33), Uzamili (13), shahada ya kwanza (4) na stashahada (4). Katika kutekeleza mradi wa "*Retooling*" unaodhamimiwa na Benki ya Dunia, Chuo kimeweza kuwapatia mafunzo walimu 500 wa masomo ya sayansi Unguja na kununua gari mbili pamoja na vifaa vya studio kwa ajili ya uazishwaji wa *SUZA TV*.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo kimefanya matengenezo mbalimbali ya majengo katika kampasi zake na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya shughuli zake za kawaida na mafeni 120 kwa ajili ya kampasi ya Tunguu. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kampasi ya Tunguu kimemaliza ujenzi wa kituo cha afya. Kituo hicho kinatarajiwa kuanza kutoa huduma zake kwa wanafunzi pamoja na wananchi waishio karibu na chuo baada ya kupokea vifaa kupitia Shirika la Kimataifa la Maendelea la Uturuki (*TIKA*).

## CHUO KIKUU CHA KUMBUKUMBU YA AL SUMAIT

Mhe. Mwenyekiti, Chuo hichi kabla kilikuwa kikijulikana kwa jina la Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Zanzibar kilichopo Chukwani na sasa kimekuwa Chuo Kikuu kamili kuanzia mwezi Julai 2014. Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Al Sumait kina jumla ya wanafunzi 1,914, kati yao 1,769 (wanawake 1,139 na wanaume 630)

wanasomea Shahada ya kwanza ya Ualimu, wanafunzi 81 wanasomea mafunzo ya Cheti na 64 Stashahada. Jadweli namba 27 inatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15, jumla ya wanafunzi 266 (wanawake 129 na wanaume 137) walihitimu masomo yao ya Shahada ya Kwanza katika fani mbali mbali. Chuo kimetoa wahitimu 1,970 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000/01. Chuo kimenunua kompyuta kwa ajili ya maktaba ya mtandao *e-library*. Maktaba hiyo ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 70 kwa wakati mmoja. Pia, Chuo kimefanya matengenezo makubwa ya kituo chake cha afya kinachotoa huduma za matibabu kwa wanafunzi, wafanyakazi na wananchi wa maeneo ya karibu. Matengenezo hayo yanalenga kukipandisha hadhi kituo hicho na kuwa na uwezo wa kutoa huduma nyingi ikiwemo upasuaji, huduma za kinamama, maabara na vipimo mbalimbali kikiwemo cha "*Ultra-sound".* Maelezo zaidi yanapatikana katiba ibara ya 98.

**CHUO KIKUU CHA ZANZIBAR**

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Chuo Kikuu cha Zanzibar kilikuwa na jumla ya wanafunzi 3,295 (wanaume 1,556 na wanawake 1,739). Kati ya hao, wanafunzi 23 wanasomea shahada ya Uzamili ya Sheria na Shariah, 74 shahada ya Uzamili ya Utawala wa Biashara, 65 shahada ya Uzamili ya Utawala wa Umma na 59 wanasomea shahada ya Uzamili ya Uchumi.

Aidha, wanafunzi 2,534 wanasomea shahada za kwanza katika fani za Biashara na Fedha, Masoko, Teknolojia ya Mawasiliano ya Kibiashara, Manunuzi, Sheria na Shari'ah, Uchumi, Utawala wa Umma, Huduma za Jamii, Teknolojia ya Mawasiliano na Elimu, Benki ya Kiislamu, Lugha na Elimu, Uhandisi wa Simu, Uhandisi wa Kompyuta na Teknolojia na Uuguzi.

Jumla ya wanafunzi 540 wanasoma katika ngazi za "*University Qualification Framework* " *Level 6,* Stashahada na Cheti katika fani za Benki ya Kiislamu na Fedha, Uhandisi wa Habari na Mawasiliano, Teknolojia ya Mawasiliano, Uhusiano wa Kimataifa, Haki ya Mtoto, Upangaji na Uendeshaji wa Miradi na Teknolojia ya Mawasiliano ya Kibiashara. Jadweli namba 28 inatoa uchambuzi zaidi. Maelezo zaidi yanapatikana katika ibara ya 100.

**BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU**

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar ni taasisi iliyopewa majukumu ya kutoa mikopo kwa wanafunzi na wafanyakazi wanaojiunga na masomo ya elimu ya juu, kufuatilia na kupokea marejesho ya mikopo hiyo kwa wahitimu. Hii ina lengo la kuendelea kuwakopesha wahitaji

wengine. Bodi pia inatafuta fursa za kielimu na ufadhili wa masomo ya elimu ya juu kutoka kwa wafadhili mbali mbali wa ndani na nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Bodi ilipanga kuwadhamini wanafunzi wapya 1,200 kujiunga na masomo ya elimu ya juu. Hata hivyo, Bodi iliwadhamini wanafunzi 1,611 sawa na ongezeko la asilimia 34 ya kiwango kilichopangwa. Wanafunzi 411 walioongezeka walitokana na nafasi za ziada za ufadhili zilizopatikana pamoja na kuanza kutumia fedha za marejesho ya madeni.

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ilifuatilia wanafunzi waliokopa ambao walipaswa kurejesha madeni baada ya kuanza kazi. Kiwango cha makusanyo kimeongezeka kutoka TSh. 249,000,000/= kwa mwaka 2013/14 na kufikia TSh. 360,000,000/= hadi Mei, 2015. Wahitimu 12 wamemaliza kulipa madeni yao kikamilifu. Hongera sana nawapongeza.

## BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Mitihani lina jukumu la kusimamia shughuli za mitihani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwemo utungaji, uchapishaji, usimamizi na usahihishaji wa mitihani ya darasa la saba, kidato cha pili na mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada ya elimu ya msingi na Stashahada ya Dini na Kiarabu. Baraza pia lina jukumu la kutathmini mwenendo mzima wa malengo ya utoaji elimu pamoja na mitihani.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, jumla ya wanafunzi 25,749 walifanya mtihani wa darasa la saba kutoka skuli za msingi 251 (152 Unguja na 99 Pemba). Kati ya wanafunzi hao, 105 walichaguliwa kujiunga na madarasa ya vipawa vya juu, ambao ni sawa na asilimia 0.4 na wanafunzi 1,558 sawa na asilimia 6.05 walifaulu na kuchaguliwa kuingia madarasa ya michepuo katika skuli mbalimbali za sekondari. Wanafunzi 24,086 wameendelea na masomo katika madarasa ya kawaida ya kidato cha kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2015 Wizara imeanza rasmi kuwashirikisha wanafunzi wa kidato cha pili wa michepuo na wa skuli binafsi. Jumla ya wanafunzi 21,944 kutoka skuli 252 (167 Unguja na 85 Pemba) walifanya mtihani huo. Kati ya wanafunzi hao, 14,384 sawa na asillimia 65.6 walifaulu na kuchaguliwa kuendelea na masomo ya kidato cha tatu. Kiwango hiki cha ufaulu kimepanda kwa asilimia 6.2 ikilinganishwa na matokeo ya mwaka 2013 ambapo asilimia ya ufaulu ilikuwa 59.4. Jadweli namba 32 linatoa ufafanuzi zaidi. Maelezo zaidi yanapatika katika ibara ya 107 hadi 110.

## BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Huduma za Maktaba ni taasisi yenye jukumu la kuanzisha, kusimamia na kusambaza huduma za maktaba katika maeneo yote ya Zanzibar. Kwa mwaka 2014/15, taasisi hii imeendelea na juhudi zake za kuhakikisha kuwa huduma za maktaba zinawafikia wananchi popote walipo, mjini na vijijini. Shirika pia, limeendelea kuihamasisha jamii kuwa na mwamko wa matumizi ya maktaba kwa ajili ya kupata maarifa ya nyanja tofauti za maisha ikiwemo elimu, biashara, utamaduni, afya na kilimo kwa kupitia programu mbalimbali zikiwemo za watoto, usambazaji vitabu skuli na katika maktaba za skuli.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika limeingiza vitabu vipya 4,482 vya watoto na watu wazima. Vitabu hivyo vimeingizwa katika maktaba kuu iliyopo Unguja na tawi lake liliopo Chake Chake Pemba. Katika jitihada za kuwawezesha watoto kuandika, kusoma na kujifunza, Shirika limeendesha programu ya watoto ndani ya maktaba kuu ya Maisara kwa Unguja na Maktaba Kuu ya Chachani Pemba. Programu hizi huendeshwa kila mwisho wa mwezi kwa kujumuisha wanafunzi 40 kutoka skuli za msingi. Vilevile, fursa iko wazi kwa skuli yoyote kuwapangia wanafunzi wao kufanya ziara za kimasomo katika maktaba. Maelezo zaidi yanapatikana katika ibara ya 113 hadi 115.

## KITENGO CHA UHASIBU

Mhe.Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/15 Kitengo kimeendelea kusimamia matumizi yote ya fedha za kawaida na fedha za maendeleo kwa mujibu wa sheria ya fedha namba 12 yamwaka 2005 na sheria ya manunuzi na uondoshaji wa vifaa chakavu namba 9 ya 2005 na kanuni zake kwa mujibu wa bajeti iliyotengwa. Aidha, Kitengo kimeimarisha utayarishaji wa ripoti ya fedha za robo mwaka pamoja na kuwasilisha ripoti ya mwaka 2013/14 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe ikiwa mnaendelea kuzungumza na sauti ya Mhe. Waziri iko chini sana, hawa watu wa *Hansard* wanapata tatizo kweli la kurikodi haya. Naomba tumsikilize Mhe. Waziri anakaribia kumaliza halafu tutawakaribisha wengine ili waweze kuendelea.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Kitengo pia, kimeendeleza mashirikiano na Wizara ya Fedha katika kutumia mtandao wa *IFMS* ambao husaidia kwa kiwango kikubwa usimamizi wa bajeti ya Wizara na hivyo kuimarisha udhibiti wa fedha za umma.

**KITENGO CHA HABARI, ELIMU NA MAWASILIANO**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15, Kitengo kiliendelea na majukumu yake ya kuratibu shughuli za utoaji wa habari sahihi za kielimu kwa jamii na kuendeleza mahusiano mazuri kati ya Wizara na Taasisi za ndani na za nje. Nimeweza kukutana na Waheshimiwa mabalozi wa nchi mbalimbali kama vile Uholanzi, Ufaransa, Comoro, Nigeria na Sweden. Pia, nilikutana na Mabalozi wadogo wa Jamhuri ya Watu wa China na Oman. Aidha, viongozi wa Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ikiwemo Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *UNICEF*, *GPE*, *SBS* – Korea, *Good Neighbors International* na *Milele Zanzibar Foundation* walifika Wizarani na kufanya nao mazungumzo kuhusu maswala mbalimbali ya kielimu. Maelezo zaidi yanapatikana katika ukurasa wa 118.

**KITENGO CHA UNUNUZI NA UGAVI**

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Ununuzi na Ugavi ni sekretariati ya Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Katika mwaka 2014/15, kitengo kwa kushirikiana na Bodi ya Zabuni kilitayarisha, kilitangaza na kuzifanyia tathmini zabuni 16 za manunuzi ya bidhaa, huduma na kazi za ujenzi zenye thamani ya jumla ya TShs. 19,288,984,112/=

**KITENGO CHA UKAGUZI WA HESABU ZA NDANI**

Mhe. Mwenyekiti, kitengo cha ukaguzi wa hesabu za ndani kina jukumu la kutoa ushauri wa matumizi ya fedha na uwekaji sahihi wa kumbukumbu na vielelezo vya matumizi katika utekelezaji wa shughuli zote za Wizara katika shughuli zote za Wizara na Taasisi zake. Ushauri huo unasaidia kuboresha na kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za Wizara na kupelekea kufikia malengo yaliyowekwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa majukumu yake mwaka 2014/15, kitengo kimezikagua Hesabu za Taasisi 2, vitengo 8 na Idara 8. Kitengo pia, kimezikagua skuli 120 (75 za Unguja na 45 Pemba) sawa na asilimia 54.5 ya lengo lililopangwa la kukagua hesabu za skuli 220. Vile vile, kitengo cha ukaguzi wa ndani kilitoa mafunzo juu ya usimamizi wa fedha kwa walimu wakuu 50, washika fedha 50 pamoja na wenyeviti wa Kamati za skuli 50 ili waweze kuweka kumbukumbu za fedha vizuri kwa mujibu wa sheria. Pia, Kitengo kiliratibu vikao vitano vya kamati ya ukaguzi wa ndani (*Audit Committee*) ambavyo vilijadili ripoti za mkaguzi wa hesabu za ndani, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mradi *wa ALSD II* na ripoti ya mkaguzi wa nje wa hesabu *(Imara Consultant* kuhusiana na mradi wa *Sida* na kupitia na kuipitisha mipango ya ukaguzi.

## KITENGO CHA URATIBU WA ELIMU YA JUU

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kiliendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya kuratibu maendeleo ya elimu ya juu, kukuza mashirikiano ya kiutendaji na Idara ya Elimu ya Juu ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Kamisheni ya Vyuo Vikuu, Vyuo vikuu na Taasisi mbalimbali zinazotoa elimu ya juu zilizopo Zanzibar na Tanzania Bara. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Kitengo kiliratibu elimu ya juu kwa kufuatilia na kutathmini utendaji kazi wa taasisi za elimu ya juu, kutangaza nafasi za masomo za nje ya Tanzania na kuweka kumbukumbu za wanaohitimu masomo yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15 nafasi za masomo kutoka China, Algeria, Uturuki, Mauritius, Urusi na Jumuiya ya Madola zilitangazwa. Jumla ya waombaji 55 walijitokeza, kati yao, 21 walifanikiwa kupata nafasi hizo. Wanafunzi 14 wamekwenda nchini China kusomea Shahada ya Uzamili, 5 Udaktari, 3 Uhandisi wa umeme, mafuta na gesi, 1 Sayansi ya mazingira, 2 Uongozi wa fedha, 1 Uongozi wa Elimu, 2 Uongozi wa Biashara na Masoko. Aidha, wanafunzi 7 wa Shahada ya Uzamili wamekwenda nchini Algeria kusomea; 2 Kemia, 2 Uhandisi wa usanifu majengo, 1 Uhandisi umeme, 1 "*Hydrocarbon*" na 1 Sayansi ya kompyuta. Waombaji 4 waliojitokeza kwa nafasi za masomo katika fani ya mafuta na gesi, Kompyuta na sayansi ya habari, Kemia na Hisabati nchini Urusi wanaendelea na mchakato huo.

Aidha, wanafunzi 16 (wanaume 07 na wanawake 09) walirejea kutoka masomoni. Kitengo kimewapatia barua za utambulisho kupeleka Tume ya Utumishi kwa ajili ya taratibu za kupatiwa ajira.

## KITENGO CHA ELIMU MJUMUISHO NA STADI ZA MAISHA

Mhe. Mwenyekiti, kitengo kina jukumu la kusimamia na kuhakikisha watoto wote wanapata elimu ya mjumuisho wakiwemo wale wenye mahitaji maalumu. Kitengo pia kina dhamana ya kuwapatia walimu, wakufunzi na wanafunzi stadi za maisha, ushauri nasaha, elimu juu ya VVU/UKIMWI, athari ya madawa ya kulevya na masuala ya jinsia ili wawe raia wema.

### Elimu Mjumuisho

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15, kitengo kimefanya ufuatiliaji na kutathmini utelekelezaji wa programu ya elimu mjumuisho katika skuli 39 (18 za Unguja na 21 za Pemba). Kitengo kimetoa mafunzo kwa wakufunzi 78 wa vyuo vitatu vya Ualimu juu ya elimu mjumuisho na mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia. Aidha, mafunzo ya nukta nundu yalitolewa kwa wanafunzi 30 wasioona (wanawake 15 na wanaume 15), na walimu 27 (9 wanaume na 18 wanawake)

wanaofundisha wasioona. Pia, mafunzo ya lugha ya alama yalitolewa kwa walimu 24 (wanaume 11 na wanawake 13) na wanafunzi viziwi na wasiokuwa viziwi 46 (21 wanaume na 25 wanawake). Mafunzo ya elimu mjumuisho na stadi za maisha yalitolewa kwa walimu 107 (28 wanaume na 79 wanawake) wa Unguja na Pemba. (Maelezo zaidi katika ibara ya 126 hadi 164).

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo kimesimamia upimaji wa wanafunzi 2,836 wenye mahitaji maalumu kwa Unguja na Pemba ili kuzitambua na kuzifanyia kazi changamoto zinazowakabili wakati wa kujifunza. Wanafunzi 8 walipatiwa rufaa kwa uchunguzi na matibabu Zaidi, wanafunzi 4 walipelekwa Mnazimmoja hospitali, 3 KCMC Moshi na 1 Muhimbili.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha taaluma ya elimu mjumuisho na kuhakikisha kuna wataalamu wa kutosha, watendaji wawili wa kitengo na wakufunzi saba wa vyuo vya Ualimu wanasomea shahada ya kwanza ya elimu mjumuisho katika vyuo vya Tanzania na Uganda. Walimu 39 (29 wanawake na 10 wanaume) wanaendelea na masomo katika fani hiyo kwa ngazi ya Diploma SUZA na walimu 44 (wanawake 41 na 3 wanaume) wapo ngazi ya Cheti katika chuo cha Ualimu - Mazizini.

Aidha, watendaji 14 wa Kitengo (8 wanawake na 6 wanaume) pamoja na walimu washauri 14 wa elimu mjumuisho wa vituo vya walimu na walimu wasaidizi (*resource teachers*) 14 wamepatiwa mafunzo ya utafiti vitendo. Mafunzo hayo yanalengo la kuwasaidia walimu kutatua changamoto wanazokumbana nazo katika utekelezaji wa elimu mjumuisho kwenye maeneo yao ya kazi. Aidha, watendaji wa Kitengo wamepatiwa mafunzo ya kufanya kazi kwa ushirikiano wa pamoja (*Team building*) kwa lengo la kurahisisha utendaji wao.

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo kimekamilisha uandaaji wa kamusi ya lugha ya alama ambalo litatumika kurahisisha mawasiliano baina ya walimu na wanafunzi viziwi na kati ya wanafunzi viziwi na wanafunzi wengine hasa katika mchakato mzima wa kufundishia na kujifunza.

**Ushauri Nasaha**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15, Kitengo kimefanya ufuatiliaji katika skuli 9 za wilaya ya Mjini kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi kujiepusha na vishawishi. Kitengo pia, kilifanya mkutano na masheha 40 wa wilaya ya Mjini kwa lengo la kupanga mikakati ya pamoja juu ya kupunguza kesi za udhalilishaji wa wanafunzi. Aidha, Kitengo kimefanya mkutano na walimu washauri wa skuli 20 za mkoa wa Mjini Magharibi wenye lengo la kujadili changamoto wanazokabiliana nazo katika kazi zao za ushauri na kuzitafutia ufumbuzi utakao wasaidia katika

kutekeleza kazi hizo kwa ufanisi mkubwa na wanafunzi kuweza kujifunza bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa walimu washauri wanafanya kazi zao kwa ufanisi, Kitengo kimefanya mkutano na viongozi 33 wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (11 wanaume na 22 wanawake) wenye lengo la kuziwasilisha changamoto za walimu washauri nasaha na kuzitafutia ufumbuzi sahihi kwa pamoja. Kitengo kinafuatilia kesi inayoendelea ya udhalilishwaji aliofanyiwa mwanafunzi wa kike wa darasa la 3 wa skuli ya Kizimkazi.

**Masuala ya Jinsia**

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha kimeendelea kutoa mafunzo kwa walimu wa skuli mbalimbali za maandalizi, msingi na sekondari ili waweze kuwaelimisha wanafunzi wa skuli zao mbinu za kuepukana na vitendo vya udhalilishaji vilivyoshamiri kwa wanafunzi. Katika mwaka 2014/15, jumla ya walimu 350 wa Unguja na Pemba (144 wanaume na 206 wanawake) walipatiwa mafunzo hayo yenye lengo la kupunguza na hatimae kuondosha kabisa vitendo vyote vya udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo, kwa kushirikiana na walimu washauri 40 (21 wanaume na 19 wanawake) kutoka skuli 40 za Unguja na Pemba kilifanya mikutano na wanafunzi wa kike wa skuli hizo lengwa. Lengo la mikutano hiyo ilikuwa ni kuwahamasisha wanafunzi wa kike waepukane na vishawishi vinavyoweza kuwapelekea kupata mimba pamoja na ndoa za mapema na badala yake waongeze bidii katika masomo yao. Jumla ya wanafunzi wa kike 6,746 walifikiwa kupitia mikutano hiyo, kati ya 2,410 ni wa skuli za msingi na 4,336 wa skuli za sekondari.

**Mapambano Dhidi ya UKIMWI na Dawa za Kulevya**

Mhe. Mwenyekiti, katika mapambano dhidi ya *VVU*/UKIMWI, Kitengo kimeandaa mafunzo ya elimu ya afya ya uzazi, UKIMWI na dawa za kulevya kwa walimu 10 wenye idadi sawa kwa jinsi zote mbili na wanafunzi 40 (20 wanawake na 20 wanaume) ambao ni waelimishaji rika na viongozi wa klabu za Afya za skuli 10 za wilaya za Kaskazini, Kusini na Magharibi. Aidha, Kamati ya UKIMWI ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilijadili changamoto za kiutendaji na kupanga mikakati ya kuzikabili changamoto hizo kwa sekta ya Elimu.

Mhe. Mwenyekiti, kongamano la kujadili changamoto zinazowakabili wanafunzi wenye mahitaji maalum katika janga la UKIMWI lilifanyika katika maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani. Jumla ya washiriki 160 walihudhuria Kongamano hilo, wakiwemo maafisa UKIMWI kutoka Wizara mbalimbali, walimu washauri, wanafunzi wenye mahitaji maalum, wajumbe kutoka jumuia ya Zapha+ na Zaca,

walimu wa klabu na wanafunzi wanaoishi na *VVU* kwa Unguja. Zoezi hili pia lilifanyika Pemba kwa kufanywa igizo la zero 3, maonyesho ya vitabu na vipeperushi mbalimbali vinavyotoa elimu ya UKIMWI na athari za unyanyapaa.

## KITENGO CHA URAJIS

### Baraza la Elimu

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Baraza la Elimu lilifanya kikao kimoja ambacho kilijadili mapendekezo ya usajili wa kudumu kwa skuli za binafsi na Serikali na taarifa za Bodi za Elimu za Mikoa yote ya Zanzibar. Wajumbe pia, walifanya ziara na kujadili maombi ya uanzishwaji wa vyuo vya ualimu vya binafsi ngazi ya cheti na Stashahada.

### Bodi za Elimu za Wilaya na Mikoa

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Bodi za Elimu za Wilaya na Mikoa zilifanya kikao kimoja kimoja. Vikao hivyo vilikuwa na lengo la kujadili maendeleo na changamoto za kielimu za ndani ya Wilaya na Mkoa husika.

### Leseni za Walimu

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, walimu 422 walipatiwa leseni za kusomeshea. Kati ya walimu hao 207 wamesomea kazi ya ualimu na 215 hawajasomea. Kitengo pia, kimefanya ukaguzi wa leseni za walimu, ufuatiliaji wa sera, sheria, kanuni na miongozo ya Wizara ya Elimu jinsi inavyofuatwa katika skuli. Kitengo kilipanga kukagua skuli 200 za Serikali na binafsi (150 Unguja na 50 Pemba). Hadi kufikia Mei, 2015, skuli 140 sawa na asilimia 70 ya lengo (44 za Serikali za Unguja na 25 Pemba na skuli 51 za binafsi Unguja na 20 za Pemba) zimekaguliwa. (Maelezo zaidi yanapatikana katika ibara ya 138 hadi 140

### Usajili wa skuli za Serikali na za Binafsi

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, skuli 17 za Serikali (moja ya maandalizi, 5 za msingi na 11 za sekondari) zimepatiwa usajili. Skuli 24 za binafsi zimewasilisha maombi ya usajili wa muda kati ya hizo, 11 za maandalizi, 11 za ngazi ya maandalizi na msingi, na 2 za ngazi ya sekondari na skuli 2 zimewasilisha maombi ya usajili wa kudumu.

### Kesi za Ujauzito na Ndoa kwa Wanafunzi

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, jumla ya kesi 9 za ujauzito kwa wanafunzi ziliripotiwa na kujadiliwa. Wanafunzi wote 9 baada ya kupatiwa ushauri

wamekubali kuendelea na masomo yao. Kitengo pia kilipokea kesi 9 za ndoa kwa wanafunzi. Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu namba 6, 1982 kifungu 20(3) wanafunzi hawa wamezuiliwa kuendelea na masomo.

**MAPATO**

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Wizara ilikadiriwa kukusanya TSh. 30,000,000/= kutoka vianzio vya ada za leseni za walimu pamoja na uandikishaji wa skuli za binafsi. Hadi kufikia Mei, 2015, jumla ya TSh. 24,731,000/= ikiwa ni sawa na asilimia 82.4 zimekusanywa na kuwasilishwa Hazina.

**MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2015/16 KATIKA MFUMO WA PROGRAMU**

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/15 naomba sasa niwasilishe vipaumbele vya Wizara na kisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2015/16 katika mfumo wa Programu.

**Vipaumbele**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2015/16**,** vipaumbele vya sekta ya elimu ni:

- Kuongeza upatikanaji wa fursa za elimu kwa usawa katika ngazi zote za elimu na mafunzo ya amali;
- Kuinua ubora wa elimu na kujenga stadi katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Katika kuchangia utekelezaji wa vipaumbele vya sekta ya elimu, Serikali imechukua hatua zifuatazo:

- Michango iliyokuwa ikitolewa na wanafunzi katika ngazi ya elimu ya msingi itafutwa rasmi kuanzia mwezi Julai 2015. Badala yake Serikali itagharimia elimu ya maandalizi na msingi kwa kuzipatia skuli na wanafunzi vifaa vya kutosha vya kusomea na kufundishia kama vile vitabu, chaki, madaftari, gharama za umeme na chakula kwa wanafunzi wa skuli za maandalizi za Serikali;(*Makofi*)
- Ada zinazotozwa kwa ajili ya Mitihani ya Taifa kwa ngazi ya elimu ya msingi na sekondari zitalipwa sasa na Serikali, hakuna tena wanafunzi kulipia gharama hizi.(*Makofi*).

- Wizara kwa kushirikiana na wadau wote wa elimu itaandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu wa muda wa miaka 5 kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2020/21. Mpango huo utaandaliwa kwa utaratibu wa Maabara. Hatua hiyo inatokana na kukaribia kumaliza muda kwa Mpango unaotekelezwa wa mwaka 2008 hadi 2016.

**Mhe. Mwenyekiti,** naomba sasa, kuwasilisha mpango wa maendeleo ya elimu kwa mwaka 2015/16 unaotumia mfumo wa Programu.

## MUUNDO WA PROGRAMU

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina programu kuu sita nazo ni;

Programu ya 1: Elimu ya Maandalizi na Msingi

Programu ya 2: Elimu ya Sekondari.

Programu ya 3: Elimu ya Juu

Programu ya 4: Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali

Programu ya 5: Ubora wa Elimu

Programu ya 6: Uongozi na Utawala

Kila programu imegawika katika programu ndogo ndogo na baadhi ya Programu zina maeneo ya utoaji huduma. Programu kuu zimeelezwa kwa umakini juu ya jina la programu na madhumuni. Kila programu ndogo au eneo la utoaji huduma linaeleza Madhumuni, Matokeo ya muda mfupi, Viashiria na Shabaha za Utekelezaji. Madhumuni yanaundwa kwa kushabihisha matokeo makuu ya programu ambayo yanaunganisha bajeti ya programu na malengo ya sera. Programu zote hizo zinatekeleza lengo la kwanza la MKUZA II kwa Klasta II la kuhakikisha usawa katika kutoa elimu bora katika jamii na jinsia.

## MAELEZO YA PROGRAMU

Mhe. Mwenyekiti, yafuatayo ni maelezo ya programu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, yanayohusisha Madhumuni, Matokeo ya muda mfupi, Viashiria na Shabaha za utekelezaji kwa kila programu.

**PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI**

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii madhumuni yake ni kumtayarisha mwanafunzi aweze kusoma, kuandika na kuhesabu. Pia programu hii ina madhumuni ya kumtayarisha mtoto kimwili na kiakili kwa ajili ya elimu ya msingi na kumuwezesha mwanafunzi aweze kusoma, kuandika na kuhesabu.

**Matokeo ya muda mfupi;**

- Kumtayarisha mtoto kwa ajili ya elimu ya msingi
- Kutoa elimu ya msingi.

**Viashiria vya matokeo;**

- Uwiyano halisi wa uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya maandalizi na msingi,
- Wastani wa mahudhurio kwa mwaka kijinsia,
- Uwiyano wa idadi ya walimu kwa nyumba za wafanyakazi katika maeneo yasiyofikika kirahisi
- Uwiyano wa wanafunzi kwa madarasa.

**Shabaha za utekelezaji;**

- Kuongeza kiwango halisi cha uandikishaji wanafunzi wa maandalizi kutoka asilimia 20.1 katika mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 30.0 ifikapo mwaka 2015
- Kuongeza kiwango halisi cha uandikishaji wanafunzi wa msingi kutoka asilimia 81.5 katika mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 95.0 ifikapo mwaka 2015.
- 

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa jumla ya Tsh. 29,261,785,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 4,879,250,000/= kwa kazi za maendeleo (kati ya fedha za maendeleo 1,000,000,000/= ni mchango wa SMZ)

**PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI**

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Elimu ya Sekondari madhumuni yake makubwa ni kumtayarisha mwanafunzi aweze kuendelea na masomo katika ngazi za juu zaidi.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Kutoa Elimu ya Sekondari
-

**Viashiria vya matokeo**

- Uwiyano wa wanafunzi wanaomaliza elimu ya lazima;
- Uwiano halisi wa undikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya kidato cha nne na cha sita;
- Uwiyano wa idadi ya walimu kwa nyumba za wafanyakazi katika maeneo yasiyofikika kirahisi; na
- Uwiyano wa wanafunzi kwa madarasa.

**Shabaha za utekelezaji**

- Kuongeza kiwango halisi cha uandikishaji wanafunzi kutoka asilimia 38.2 katika mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 60.0 ifikapo mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Elimu ya Sekondari. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, programu hii imepangiwa jumla ya Tsh**.** 20,044,323,000/= kwa kazi za kawaida na Tsh. 1,000,000,000/= kwa kazi za maendeleo ambazo ni mchango wa SMZ.

**PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU**

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujiajiri au kuajiriwa**.** Programu hii ina programu ndogo moja na maeneo madogo manne ambayo ni:-

**Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu**

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina madhumuni ya kuwawezesha wanafunzi kuwa wabunifu, wataalamu na wenye uwezo wa kuongoza ili kukuza ubora wa elimu.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Elimu ya Diploma ya Ualimu kutolewa

**Viashiria vya matokeo**

- Idadi ya wanafunzi wote walio katika vyuo

**Shabaha za Utekelezaji**

- Kuongeza kiwango cha asilimia ya walimu wenye sifa kutoka asilimia 94 mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 98 mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Mafunzo ya Ualimu. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa jumla ya TSh. 1,215,160,000/= kwa kazi za kawaida.

**Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti**

Mhe. Mwenyekiti, Huduma hii ina madhumuni ya kumtayarisha mwanafunzi kuingia katika fani za kitaalamu na ajira.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Kiwango cha elimu ya Stashahada, Shahada ya kwanza, Shahada ya pili na Shahada ya tatu kutolewa.

**Viashiria vya matokeo**

- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza ngazi ya stashahada;
- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza ngazi ya Stashahada ya uzamili;
- Shahada ya kwanza, ya pili na ya tatu; na
- Idadi ya tafiti zinazofanywa.

**Shabaha za Utekelezaji**

- Kuongeza idadi ya wanafunzi wa Chuo Kikuu kutoka 3,624 mwaka 2014 hadi kufikia 6,000 mwaka 2015
-

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za Huduma hii zinatekelezwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Kwa mwaka wa fedha 2015/16, huduma hii imepangiwa ruzuku ya TSh. 5,207,000,000/=

**Huduma ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia**

Mhe. Mwenyekiti, Huduma hii ina madhumuni ya kuimarisha elimu ya sayansi na teknolojia.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Ufundishaji na kujifunza Sayansi, Hisabati na Teknolojia; na
- Ufundi kuimarishwa.

**Viashiria vya matokeo**

Idadi ya wanafunzi wahitimu katika taasisi; na

- Uwiyano wa wanafunzi kwa madarasa.

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za Huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa ruzuku ya Tsh. 976,000,000/=

**Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu**

Mhe. Mwenyekiti, Huduma hii ina madhumuni ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya Juu.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutolewa**.**

**Viashiria vya matokeo**

- Idadi ya wanafunzi wanaopokea mikopo

**Shabaha za Utekelezaji**

- Kuongeza utowaji wa mikopo kwa wanafunzi kutoka asilimia 10 mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 30 ifikapo mwaka 2015; na
- Kukusanya angalau asilimia 25 ya mikopo iliyotolewa kwa wanafunzi ifikapo mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa ruzuku ya Tsh. 8,259,000,000/=.

**Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu**

Mhe. Mwenyekiti, Huduma hii ina madhumuni ya usimamizi na tathmini ya elimu ya juu.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Tathmini ya elimu ya juu katika vyuo vinavyotoa elimu ya juu kufanyika

**Viashiria vya matokeo**

- Idadi ya wanafunzi wanaoendelea na masomo ya elimu ya juu kijinsia

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya juu. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa jumla ya Tsh. 30,000,000,/= kwa kazi za kawaida.

**PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI**

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu ya mafunzo ya amali kwa mwanafuzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira. Programu hii ina programu ndogo ndogo mbili kama ifuatavyo;

**Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali**

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu itakayowawezesha vijana kujiajiri ili kujikwamua na umasikini.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Mafunzo ya Amali na ufundi kutolewa

**Viashiria vya matokeo**

- Ukosefu wa ajira kwa vijana kupungua; na
- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza mafunzo ya amali kuongezeka.

**Shabaha za utekelezaji**

- Kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana kutoka kiwango cha asilimia 19.6 kwa mwaka 2009 hadi asilimia 11.4 ifikapo mwaka 2015

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, Mamlaka imetengewa ruzuku ya TSh. 1,356,000,000/= kwa kazi za kawaida.

**Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima**

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina madhumuni ya kupunguza kiwango cha kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu miongoni mwa wanajamii.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Elimu mbadala na ya watu wazima kutolewa

**Viashiria vya matokeo**

- Kiwango cha kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa watu wazima;
- Idadi ya watu wazima wanaoshiriki katika madarasa ya wanakisomo; na
- Idadi ya vijana waliojiunga na madarasa na vituo vya elimu mbadala.

**Shabaha za Utekelezaji**

- Kuongeza kiwango cha kujua kusoma na kuandika kutoka Asilimia 75.8 mwaka 2005 hadi kufikia asilimia 90 ifikapo mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imetengewa jumla ya Tsh. 788,969,000/= kwa kazi za kawaida na TSh**.** 18,019,250,000/= kwa kazi za maendeleo (kati ya fedha za maendeleo TSh. 500,000,000/= ni mchango wa SMZ).

**PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU**

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu, ina programu ndogo ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama yafuatayo.

**Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia**

Mhe. Mwenyekiti, Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za maandalizi, msingi, sekondari na mafunzo ya Ualimu.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Mitaala ya Elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi zote kutayarishwa.

**Viashiria vya matokeo**

- Idadi ya Mitaala na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi zote kutayarishwa.

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za utowaji wa huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Elimu Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Taasisi imetengewa ruzuku ya TSh. 87,880,000/= kwa kazi za kawaida.

**Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu**

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utekelezaji wa utoaji wa elimu.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Malengo ya elimu kupimwa

**Viashiria vya matokeo**

- Asilimia ya walimu wenye sifa; na
- Asilimia ya wanafunzi na kiwango cha mpito katika ngazi za darasa la sita, kidato cha pili, kidato cha nne na cha sita kupimwa.

**Shabaha za Utekelezaji**

- Kuongeza kiwango cha asilimia ya walimu wenye sifa kutoka asilimia 94 mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 98 mwaka 2015 katika ngazi zote za elimu;
- Kiwango cha mpito kutoka kidato cha pili kwenda cha tatu kuongezeka kutoka asilimia 58.2 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 70 ifikapo mwaka 2015; na
- Kiwango cha mpito kutoka kidato cha nne kwenda cha tano kuongezeka kutoka asilimia 23.3 mwaka 2009 hadi asilimia 50 ifikapo mwaka 2015.
- 

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa ruzuku ya Tsh. 1,508,000,000/=.

**Huduma ya Ukaguzi wa Elimu**

Mhe. Mwenyekiti, utoaji wa huduma hii una madhumuni ya kusimamia utoaji wa elimu unaofuata mtaala na kuhakikisha ufanisi na ubora wa elimu.

**Viashiria vya matokeo**

- Idadi ya skuli zilizokaguliwa; na
- Idadi ya ripoti za ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa ruzuku ya Tsh. 106,000,000/= kwa kazi za kawaida.

**Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha**

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu kwa wote wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa watoto wenye mahitaji maalum kutolewa
-

**Viashiria vya matokeo**

- Idadi ya wanafunzi na walimu katika Elimu Mjumuisho.

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, Kitengo kimepangiwa kutumia jumla ya Tsh 60,000,000,/= kwa kazi za kawaida.

**Huduma za Maktaba**

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina madhumuni ya kutoa fursa ya kutumia vitabu na vyanzo vyengine vya taaluma kwa wananchi.

**Matokeo ya muda mfupi**

Kutoa nafasi kwa wanafunzi na watu wengine ya kupata taarifa mbalimbali kupitia maktaba.

**Viashiria vya matokeo**

- Idadi ya watu wanaotumia maktaba;
- Idadi ya vitabu, CDs, magazeti na majarida yaliyopo katika maktaba; na
- Idadi ya skuli zilizokuwa na maktaba kamili.

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa kutumia ruzuku ya Tsh 365,000,000/= kwa kazi za kawaida.

**Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*ICT*)**

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina madhumuni ya kuifanya teknolojia ya habari na mawasiliano itumike katika kujifunza, kufundisha na ngazi ya utawala na katika maisha ya kila siku.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Walimu wanapatiwa mafunzo juu ya matumizi ya Teknolojia ya kisasa.

**Viashiria vya utekelezaji**

- Idadi ya walimu wenye ujuzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;
- Idadi ya vifaa vya Teknolojia ya Habari na mawasiliano katika skuli na Wizara;
- Idadi ya Taasisi za elimu zilizounganishwa na mkonga wa Taifa; na
- Mafunzo ya matumizi ya kompyuta kutolewa kuanzia katika skuli za msingi.

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Katika Elimu. Katika mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya Tsh 387,600,000/= kwa kazi za kawaida.

**Huduma ya Urajisi wa Elimu**

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina madhumuni ya kuhakikisha Sheria, Sera na taratibu za Wizara zinafuatwa. Pia kutoa leseni kwa walimu na kusajili skuli za Serikali na za binafsi.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Skuli za serikali na binafsi zenye viwango bora kusajiliwa; na
- Leseni za walimu kutolewa.

**Viashiria vya matokeo**

- Idadi ya leseni za walimu;
- Idadi ya skuli zilizosajiliwa; na
- Sheria ya Elimu inapitiwa na kurekebishwa.

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za utowaji wa huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mrajisi wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TSh. 47,000,000/= kwa kazi za kawaida.

**Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli**

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mwanafunzi kimwili, kiafya na kiakili katika kujifunza kwa kupitia michezo.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Kuinua taaluma ya michezo katika skuli.

**Viashiria vya matokeo;**

- Idadi ya walimu wenye taaluma ya michezo;
- Idadi ya viwanja vya michezo kwa watoto; na
- Idadi ya vifaa vya michezo kwa wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Michezo na Utamaduni katika skuli. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya Tsh 271,022,000/= kwa kazi za kawaida.

**PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI**

Mhe. Mwenyekiti, programu hii madhumini yake makubwa ni kuhakikisha nyenzo zilizo bora zinapatikana na zinatumika kwa kuimarisha utoaji wa elimu**.** Programu hii ina programu ndogo mbili kama ifuatavyo:-

**Programu ndogo ya Uongozi kiujumla**

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina madhumuni ya kutoa ufanisi wa Uongozi na utawala wa rasilimali za Wizara.

**Matokeo ya muda mfupi**

- Kupatikana kwa Ufanisi wa Uongozi na Utawala wa Rasilimali za Wizara.

**Viashiria vya matokeo**

- Idadi ya wafanyakazi wanaoajiriwa na kustaafu; na
- Mafunzo yanayotolewa kwa wafanyakazi**.**

**Shabaha za Utekelezaji**

- Kukuza ufanisi katika kutoa huduma kwa wafanyakazi na upatikanaji wa nyenzo za kufanyia kazi.
-

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TSh. 2,187,521,000/= kwa kazi za kawaida.

**Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti**

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina madhumuni ya kufanikisha na kuratibu Mipango, Sera na Utafiti katika Wizara.

**Matokeo ya muda mfupi**

Kupatikana kwa sera na mipango ya Wizara, kufanya utafiti, na kufanya ufuatiliaji na tathmini.

**Viashiria vya matokeo**

- Idadi za tafiti zilizofanywa pamoja; na
- Ripoti za utekelezaji na ripoti za tathmini.
-

Mhe. Mwenyekiti, Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Sera, Mipango na Utafiti. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TSh. 2,269,916,000/= kwa kazi za kawaida.

**Programu ndogo ya kuratibu shughuli za elimu Pemba**

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina madhumuni ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za elimu kwa upande wa Pemba. Matokeo ya muda mfupi na shabaha za utekelezaji zinazotumika ni kama zile zilizoelezwa katika programu za hapo juu.

Mhe. Mwenyekiti, msimamizi wa shughuli za programu hii ni Afisa Mdhamini wa Wizara yangu kupitia katika Divisheni ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi Pemba**.**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/16, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya Tsh. 22,427,724,000/= kwa kazi za kawaida.

**MGAWANYO WA FEDHA KWA PROGRAMU**

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu hii inaonesha mgawanyo wa fedha kwa Programu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yenye kuzingatia gharama za Idara/Vitengo/Taasisi zilizomo katika programu husika.

**Programu 1: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI**

**Idara Husika:** Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi

**Gharama za Programu**

Jumla ya shilingi 34,141,035,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii. Kati ya fedha hizo, shilingi 29,261,785,000/= ni kwa kazi za kawaida na shilingi 4,879,250,000/= kwa kazi za maendeleo.

**Programu Pili: ELIMU YA SEKONDARI**

**Idara Husika:** Idara ya Elimu ya Sekondari

**Gharama za Programu**

Jumla ya shilingi 21,044,323,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii. Kati ya fedha hizo, shilingi 20,044,323,000/= ni kwa kazi za kawaida na shilingi 1,000,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

**Programu Tatu: ELIMU YA JUU**

**Taasisi Husika**

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, Mafunzo ya Ualimu, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Kitengo cha Uratibu wa Elimu wa Juu.

**Gharama za Programu**

Jumla ya shilingi 15,685,160,000/= zimepangwa kwa kufanikisha programu hii kwa kazi za kawaida.

**Programu Nne: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI**

**Idara Husika**

Mamlaka ya mafunzo ya Amali pamoja na Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima.

**Gharama za Programu**

Jumla ya shilingi 20,164,219,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,144,969,000/= ni kwa kazi za kawaida na shilingi 18,019,250,000/= kwa kazi za maendeleo.

**Programu Tano: UBORA WA ELIMU**

**Idara Husika**

Taasisi ya Elimu Zanzibar, Baraza la Mitihani la Zanzibar, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar, Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Katika Elimu, Ofisi ya Mrajisi wa Elimu, Idara ya Michezo na Utamaduni Katika Skuli.

**Gharama za Programu**

Jumla ya shilingi 2,806,502,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii kwa kazi za kawaida.

**Programu Sita: UONGOZI NA UTAWALA**

**Idara Husika**

Idara ya Utumishi na Uendeshaji na Idara ya Mipango Sera na Utafiti.

**Gharama za Programu**

Jumla ya shilingi 26,885,161,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii kwa kazi za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, mapato ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yanatokana na utoaji wa leseni za walimu nausajili wa skuli binafsi. Kwa mwaka wafedha 2015/16 Wizara yangu inakusudia kukusanya Tsh. 24,713,000/=.

**JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

Mhe. Mwenyekiti, gharama kwa programu zote sita za Wizara ni shilingi 120,726,400,000/=, sawa na bajeti yote ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inayotumia programu iliyoainishwa Barazani. Kati ya fedha hizo, 96,827,900,000/= zimetengwa kwa kazi za kawaida na 23,898,500,000/= kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, shilingi 2,900,000,000/= ni mchango wa SMZ na Shilingi 20,998,500,000/= ni mchango wa Wahisani.

**SHUKRANI**

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukurani za dhati kwa washirika wote wa sekta ya elimu wakiwemo wananchi, washirika wa maendeleo na mashirika ya misaada ya kimataifa kwa kutunga mkono katika jitihada zetu za kuendeleza elimu.  Tunatoa shukurani zetu za pekee kwa Serikali ya Sweden, Marekani, Oman na Serikali ya Watu wa China, India na Misri. Pia, napenda kuyashukuru mashirika mbali mbali yakiwemo, Sida, *USAID*, *UNESCO*, *UNICEF*, *ILO*, *VSO*, *OPEC Fund*, *GPE* na *Partnership for Child Development* kupitia *Imperial College of Science and Technology (UK).*  Pia shukurani zetu za dhati kwa Aga Khan Foundation, Benki ya Dunia, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Napenda pia, kuyashukuru mashirika yasio ya kiserikali yakiwemo Milele Zanzibar Foundation, *ZAYADESA*, *NFU*, FAWE, Save the Children Fund, Book Aid International na ZAPDD. Vile Vile napenda kuyashukuru makampuni na mashirika mbali mbali ya kifedha kama vile *ZTE*, Benki ya watu wa Zanzibar, *CRDB*, *NBC*, Postal Bank, *ZANTEL*, Tigo kwa misaada yao kwa sekta ya elimu.

Mwisho, napenda kutoa shukrani zangu kwa viongozi wenzangu kuanzia wewe Mheshimiwa Spika na wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa walionipa na kwa namna watakavyoichangia hotuba yangu hii. Nasema ahsanteni sana. Pia napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Donge kwa kunipa heshima ya kuwatumikia na ushirikiano mkubwa walionipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya jimbo na ya kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makadirio ya matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya jumla ya Shilingi 120,726,400,000/= kwa mwaka wa fedha 2015/16, ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Asante Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wako. Waheshimiwa Wajumbe hotuba hii ya Mhe. Waziri katika bajeti hii imekwisha kuungwa mkono, sasa tumkaribishe Mwenyekiti.

**UTARATIBU**

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara ya Elimu ni miongoni mwa Wizara muhimu sana. Na kwa kuwa Mhe. Waziri ametumia karibu takriban masaa mawili na nusu katika kuwasilisha hotuba yake, nadhani isingekuwa vyema kuipa Kamati dakika 15 kuwasilisha taarifa hii.

Napenda nichukue fursa hii Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu kabisa, umtake Waziri wa Wanchi katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais atumie Kanuni au Mwanasheria Mkuu wa Serikali atumie kanuni ya kuahirisha Baraza hili kabla ya Wakati wake, kusudi Mhe. Mwenyekiti, Jumatatu tukijaaliwa Mwenyekiti wa Kamati aweze kupata angalau saa moja na yeye kutoa maoni ya Kamati.

Asante sana Mheshimiwa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Asante Mhe. Mjumbe kwa umakini wako. Sasa basi tumpishe Mhe. Mwanasheria Mkuu ili aje kutoa hoja.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Saleh Nassor Juma alishatoa hoja, sasa mimi niombe kutenga kando tu Kanuni ya muda ili tuahirishe Kikao hiki kama ambavyo imetolewa hoja hadi siku ya Jumatatu saa 3:00 asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe wale wanaounga mkono hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wanyooshe mkono. Wanaopinga, waliokubali wameshinda.

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*

*(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru sana kwa namna tulivyoshirikiana pamoja hadi kufikia hatua hii sasa hivi. Lakini kabla hatujaahirisha Baraza letu hili kuna tangazo ambalo tumeletewa na Mhe. Spika.

Mhe. Spika, wa Baraza la Wawakilishi anawatangazia Waheshimiwa Wajumbe wote na kuwakumbusha kwamba wasisahau kesho kuhudhuria katika Semina inayohusu usafiri wa barabarani itakayofanyika hapa kesho, siku ya Jumamosi tarehe 6/6/2015 katika ukumbi wetu wa hapo juu. Waheshimiwa wote mnasisitizwa kuhudhuria kwa wingi kuanzia saa 2:00 -2:30 muwe mmefika nyote. Shime nyote muje mapema ili tumalize mapema tuendelee na masuala mengine.

Baada ya tangazo hilo sasa kwa mara nyengine tena nizidi kukushukuruni tena. Pia napenda kuchukua fursa hii sasa kuahirisha Baraza hili hadi siku ya Jumatatu tarehe 08/06/2015 saa 3:00 za asubuhi. Naomba kuahirisha.

*(Saa 1:31usiku Baraza liliahirishwa hadi*

*tarehe* 08/06/2015 asubuhi saa 3:00)